BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR 2016 - 2020

	1.	Mhe. Zubeir Ali Maulid	-	SPIKA
2.	Mhe.	Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
3.	Mhe.	Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4.	Mhe.	Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
5.	Mhe.	Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
6.	Mhe.	Issa Haji Ussi Gavu	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
7.	Mhe.	Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
8.	Mhe.	Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
9.	Mhe.	Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais /Uteuzi wa Rais
10.	Mhe.	Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
11.	Mhe.	Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii, na Mambo ya Kale/Jimbo la Kiembesamaki
12.	Mhe.	Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
13.	Mhe.	Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, na Viwanda / Uteuzi wa Rais
14.	Mhe.	Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo/ Uteuzi wa Rais
15.	Mhe.	Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Amani

16.	**Mhe. Hamad Rashid Mohamed**	**-**	**MBM/Waziri wa Afya / Uteuzi wa Rais**
17.	**Mhe. Maudline Cyrus Castico**	**-**	**MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais**
18.	**Mhe. Salama Aboud Talib**	**-**	**MBM/Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati / Nafasi za Wanawake**
19.	**Mhe. Sira Ubwa Mamboya**	**-**	**MBM/ Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais**
20.	**Mhe. Juma Ali Khatib**	**-**	**MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais**
21.	**Mhe. Said Soud Said**	**-**	**MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais**
22.	**Mhe. Khamis Juma Mwalim**	**-**	**Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe**
23.	**Mhe. Mihayo Juma N'hunga**	**-**	**Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais /Jimbo la Mwera**
24.	**Mhe. Shamata Shaame Khamis**	**-**	**Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Micheweni**
25.	**Mhe. Harusi Said Suleiman**	**-**	**Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete**
26.	**Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri**	**-**	**Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani**
27.	**Mhe. Mohamed Ahmada Salum**	**-**	**Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/Jimbo la Malindi**
28.	**Mhe. Chum Kombo Khamis**	**-**	**Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale/ Nafasi za Wanawake**
29.	**Mhe. Shadya Mohamed Suleiman**	**-**	**Naibu Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake**
30.	**Mhe. Lulu Msham Abdalla**	**-**	**Naibu Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo/ Nafasi za Wanawake**
31.	**Mhe. Juma Makungu Juma**	**-**	**Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba , Maji na Nishati / Jimbo la Kijini**
32.	**Mhe. Hassan Khamis Hafidh**	**-**	**Naibu Waziri wa Biashara, na Viwanda /Jimbo la Welezo**
33.	**Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi**	**-**	**Naibu Waziri wa Kilimo,**

				Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mtopepo
34.	**Mhe.**	**Abdalla Ali Kombo**	**-**	**Jimbo la Mwanakwerekwe**
35.	**Mhe.**	**Ali Khamis Bakar**	**-**	**Jimbo la Tumbe**
36.	**Mhe.**	**Ali Salum Haji**	**-**	**Jimbo la Kwahani**
37.	**Mhe.**	**Ali Suleiman Ali (Shihata)**	**-**	**Jimbo la Kijitoupele**
38.	**Mhe.**	**Ahmada Yahya Abdulwakil**	**-**	**Uteuzi wa Rais**
39.	**Mhe.**	**Ame Haji Ali**	**-**	**Jimbo la Nungwi**
40.	**Mhe.**	**Amina Iddi Mabrouk**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
41.	**Mhe.**	**Asha Abdalla Mussa**	**-**	**Jimbo la Kiwengwa**
42.	**Mhe.**	**Bahati Khamis Kombo**	**-**	**Jimbo la Chambani**
43.	**Mhe.**	**Bihindi Hamad Khamis**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
44.	**Mhe.**	**Hamad Abdalla Rashid**	**-**	**Jimbo la Wawi**
45.	**Mhe.**	**Hamida Abdalla Issa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
46.	**Mhe.**	**Hamza Hassan Juma**	**-**	**Jimbo la Shaurimoyo**
47.	**Mhe.**	**Hidaya Ali Makame**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
48.	**Mhe.**	**Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)**	**-**	**Jimbo la Mtoni**
49.	**Mhe.**	**Jaku Hashim Ayoub**	**-**	**Jimbo la Paje**
50.	**Mhe.**	**Khadija Omar Kibano**	**-**	**Jimbo la Mtambwe**
51.	**Mhe.**	**Machano Othman Said**	**-**	**Jimbo la Mfenesini**
52.	**Mhe.**	**Makame Said Juma**	**-**	**Jimbo la Kojani**
53.	**Mhe.**	**Maryam Thani Juma**	**-**	**Jimbo la Gando**
54.	**Mhe.**	**Masoud Abrahman Masoud**	**-**	**Jimbo la Bububu**
55.	**Mhe.**	**Miraji Khamis Mussa**	**-**	**Jimbo la Chumbuni**
56.	**Mhe.**	**Moh'd Mgaza Jecha**	**-**	**Jimbo la Mtambile**
57.	**Mhe.**	**Mohamed Said Mohamed**	**-**	**Jimbo la Mpendae**
58.	**Mhe.**	**Mohammedraza Hassanaali Mohamedali**	**-**	**Jimbo la Uzini**
59.	**Mhe.**	**Mtumwa Peya Yussuf**	**-**	**Jimbo la Bumbwini**
60.	**Mhe.**	**Mtumwa Suleiman Makame**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
61.	**Mhe.**	**Mussa Ali Mussa**	**-**	**Jimbo la Ole**
62.	**Mhe.**	**Mussa Foum Mussa**	**-**	**Jimbo la Kiwani**
63.	**Mhe.**	**Mwanaidi Kassim Mussa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
64.	**Mhe.**	**Mwantatu Mbaraka Khamis**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
65.	**Mhe.**	**Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini**	**-**	**Jimbo la Dimani**
66.	**Mhe.**	**Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy**	**-**	**Jimbo la Chaani**
67.	**Mhe.**	**Nassor Salim Ali**	**-**	**Jimbo la Kikwajuni**
68.	**Mhe.**	**Omar Seif Abeid**	**-**	**Jimbo la Konde**
69.	**Mhe.**	**Panya Ali Abdalla**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
70.	**Mhe.**	**Rashid Makame Shamsi**	**-**	**Jimbo la Magomeni**
71.	**Mhe.**	**Saada Ramadhan Mwendwa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
72.	**Mhe.**	**Said Omar Said**	**-**	**Jimbo la Wingwi**
73.	**Mhe.**	**Said Hassan Said**	**-**	**Mwanasheria Mkuu**
74.	**Mhe.**	**Salha Mohamed Mwinjuma**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
75.	**Mhe.**	**Salma Mussa Bilal**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
76.	**Mhe.**	**Shaib Said Ali**	**-**	**Jimbo la Chonga**
77.	**Mhe.**	**Simai Mohammed Said**	**-**	**Jimbo la Tunguu**
78.	**Mhe.**	**Suleiman Makame Ali**	**-**	**Jimbo la Ziwani**
79.	**Mhe.**	**Suleiman Sarahan Said**	**-**	**Jimbo la Chakechake**
80.	**Mhe.**	**Tatu Mohamed Ussi**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
81.	**Mhe.**	**Ussi Yahya Haji**	**-**	**Jimbo la Mkwajuni**

82.	**Mhe.**	**Viwe Khamis Abdalla**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
83.	**Mhe.**	**Wanu Hafidh Ameir**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
84.	**Mhe.**	**Yussuf Hassan Iddi**	**-**	**Jimbo la Fuoni**
85.	**Mhe.**	**Zaina Abdalla Salum**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
86.	**Mhe.**	**Zulfa Mmaka Omar**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
	Ndg. Raya Issa Msellem		**-**	**Katibu**

Kikao cha Kumi na Nane – Tarehe 01 Juni, 2018

Kikao Kilianza Saa 3:00 Asubuhi

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Shehe Hamad Mattar) alisoma dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe katika kikao cha tarehe 13 Februari, 2018, Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa aliuliza swali la nyongeza kwa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto lililotokana na swali la msingi Nam. 14. Aidha, katika kikao cha tarehe 28 Februari, 2018 Mhe. Asha Abdalla Mussa aliuliza swali la nyongeza lililotokana na swali la msingi Nam. 56. Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto aliahidi kujibu maswali hayo kwa maandishii.

Sasa namuomba Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto asome majibu ya maswali ya nyongeza yaliyoulizwa na Wajumbe hao.

Mhe. Naibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti**,** kwa ruhusa yako naomba kutoa jibu la maandishi lililotokana na swali la nyongeza la Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa swali lake kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, walengwa wakubwa wa Mfuko wa Uwezeshaji ni wanawake na Vijana. Kutokana na kuanzishwa kwa Mabaraza ya Vijana, Wizara kupitia Mfuko wa Uwezeshaji imebuni mikakati ya kuyapatia mitaji Mabaraza hayo ili kuanzisha na kuendeleza miradi mbali mbali ya kiuchumi Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na upya wa Mabaraza haya ya Vijana, Wizara imekuwa ikiwasaidia mitaji vijana kupitia vikundi vyao vya uzalishaji vilivyomo katika Wilaya zote za Unguja na Pemba hadi hapo Mabaraza hayo

yatakapokamilisha mambo ya msingi ikiwemo miradi ya kiuchumi watakayoitekeleza.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka huu wa 2017/2018 hadi mwezi Aprili, 2018 jumla ya vikundi 10 vya vijana vilivyomo katika Wilaya tatu za Mkoa wa Mjini/Magharibi vilisaidiwa mikopo ya uwezeshaji ambapo jumla ya Tshs.41,000,000/- zilitolewa na vikundi hivyo ni kama ifuatavyo:
Jina la Kikundi

1. Hamasika drop Mwanakwerekwe Magharibi (B) shughuli wanayofanya ni biashara Mil. 5

2. Lam drop, Chukwani Magharibi (B) biashara ni nafaka Mil. 3

3. Damaunt, Kwarara Magharibi (B) uchimbaji wa visima Mil. 4

4. Chapakazi, Mwanakwerekwe Magharibi (B) vifaa vya elimu Mil. 3

5. Yasin *Business group*, Nyerere, biashara Mil. 4

6. Kaangoni *group*, Mbuzini Magharibi (A) seremala Mil. 4

7. Rubeya *surprise* ,Welezo Magharibi (A) ufugaji Mil. 4

8. *Uhuru Enterprise group*, Mwera Magharibi (A) vifaa vya elimu Mil. 3,500,000

9. *Rukiya business group*, Mkunazini Mjini, Duka la chakula Mil. 3

10. *Zeyana business group* Kiponda Mjini, Duka nguo na chakula Mil. 7,500,000

Mhe. Mwenyekiti, aidha, naomba kumjibu Mhe. Asha Abdalla Mussa swali lake la nyongeza alilotaka kujua. Je, kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara ilijipangia kukusanya jumla ya shilingi ngapi kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti**,** kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara imejipangia kukusanya shilingi Milioni Mia Nane Tisini na Moja Elfu Sabini na Nane

(891,078,000/-) hadi kufikia Aprili, 2018 Wizara tayari imeshakusanya jumla ya Tanzania shilingi Milioni Mia Sita Sitini na Sita Laki Tisa Arubaini na Nane Elfu Mia Sita na Tisini (666,948,690/-) sawa na asilimia Sabini na tano (75%) ya lengo lililowekwa.

Aidha, Wizara kwa mwaka ujao wa fedha 2018/2019 imejipangia kukusanya jumla ya shilingi Milioni Saba Tisini na Nne Laki Sita na Elfu Kumi na Tatu (794,613,000/-).

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kuhusu utaratibu Mhe. Mwenyekiti. Nimesimama Kanuni ya 63 (43) sijui utaniruhusu kusoma au itakuwa imekidhi

Mhe. Mwenyekiti: kisome ili kieleweke

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti,

> "Kiongozi wa shughuli za serikali au Waziri yeyote anaweza kutoa kauli katika Baraza kuhusu jambo lolote ambalo serikali inawajibika na baada ya hapo Mwenyekiti wa Kamati inayohusika au Mjumbe mwengine aliyeidhinishwa na Kamati anaweza kupewa nafasi ya kutoa maoni ya Kamati juu ya kauli hiyo"

Mhe. Mwenyekiti, pana jambo limechukua muda mrefu. Zanzibar inategemea uchumi wake kutoka zao la karafuu, pili ni utalii. Pana barabara yetu kati kati hapa Kiembesamaki, hata viongozi wetu wakuu akiwemo Mhe. Rais, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Balozi akija hapa Barazani ile njia inasumbua muda mrefu na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji haijachukua hatua yoyote mpaka muda huu. Hata juzi tulipokea mgeni Waziri wa kutoka Saudia Arabia haileti taswira nzuri ile barabara kusema ukweli.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka Kauli ya Serikali kuhusu shimo lile au barabara ile.

Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Jaku Hashim Ayoub umesikika na serikali imesikia.

HOJA ZA SERIKALI

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe hoja inaendelea kujadiliwa lakini niwaambie kwamba niombe sana sana wachangiaji wetu bado ni wengi tuna wachangiaji hapa kama ilivyotolewa jana, na siku yetu leo ni ya Ijumaa tuna masaa machache sana. Kwa hivyo niwaombeni sana itabidi wale waliochangia, walioleta orodha yao kwa hapa mbele ya meza itabidi wajitayarishe kama walivyoambiwa jana kuchangia kwa maandishi, nitawapa wachache sana na kwa muda wa dakika 10, nitatoa Wajumbe watatu tu ili tuweze kumpa Mhe. Naibu Waziri, Mhe. Waziri na wao kuweza kuchangia na kuweza pamoja kujibu hoja zetu ambazo kuwa zimeletwa. Kwa hivyo naomba sana muwe wavumilivu kwa hayo ili jambo hili liweze kumaliza leo. Ahsanteni.

UTARATIBU

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Kuhusu utaratibu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante kuhusu utaratibu

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, nazungumzia kwenye Kifungu cha 58(6) na ninaomba niisome

> "Kila Mjumbe anayejadili hoja ataruhusiwa kusema kwa muda usiozidi dakika 15 wakati wa mikutano ya kawaida na dakika 20 katika wakati wa mikutano ya bajeti lakini Spika au Mwenyekiti akiona inafaa ataweza kumuongeza msemaji dakika sio zaidi ya 10".

Mhe. Mwenyekiti, hapa nilikuwa narudia hii kauli ambayo kiti chako kimetuongoza na mimi nakiheshimu sana kuwa watu ambao wamepata wazungumze si chini ya dakika 10. Hii itakuwa ni uonevu au la kiti chako kiamrishe kulihoji Baraza letu hili kikubaliane na muda huo itengue Kanuni ya Muda ili tuone basi haki inapatikana kwa Wajumbe.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kwa mnasaba huo sisi tumekuja hapa hatukuja kuandika, tumekuja kwa kuzungumza moja kwa moja ili wananchi waone jinsi gani tunavyowatetea. Mhe. Mwenyekiti, hili ndio nililotaka niombe kiti chako kiangalie hiyo dakika 10 kuwa haitoshi.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mohamed Said Mohamed nimekusikia ni kweli Kanuni inasema hivyo lakini na kiti pia vile vile kina nafasi yake, lakini kulingana na hali ilivyo hatuwezi kama leo tuongeze muda turudi tena baada ya Sala ya Ijumaa, ndio ikawezekana kwamba tufanye busara Wizara hii leo imalize ili saa 6 tuweze kwenda kusali na tusirejee tena. Niwaombe tena sana, huu muda wa dakika 10 mtu aende moja kwa moja kwenye hoja yake ya msingi ili jambo hili liweze kumaliza.

Nawaombeni sana.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, napata ukakasi mkubwa sana kuwa hii Kanuni tulikuwemo humu huitaki au unaipinda, najua kiti chako kina amri ya kuongeza dakika lakini si kupunguza. Sasa kama ni kupunguza turudi kwenye Baraza tuliambie Baraza basi tutengue Kanuni na Wajumbe wakubali kuwa tukubali dakika 10 ili turidhie kiti chako na Baraza turidhie. Kwa sababu hii Kanuni ndio inayotumika humu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mohamed Said Mohamed pamoja na kuwa ni hivyo unavyoeleza lakini ni bado busara inatakiwa itumike kwenye kiti. Kwa hivyo busara yangu ni kwamba tuutumie tutaweza kufanya yale ambayo tumeyakusudia. Hivyo Katibu tuendelee.

Sasa naomba nimwite mchangiaji Mhe. Omar Seif Abeid na akifuatia Mhe. Miraji Khamis Mussa ajitayarishe. *(Makofi).*

Mhe. Omar Seif Abeid:Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru samahani nilikuwa sijasikia, sikusikia vizuri kutokana na hali yenyewe ilivyo lakini nakushukuru kunipa nafasi ya kwanza katika kuchangia Wizara hii ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, wizara muhimu.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote na mimi sina budi kumshuru Mwenyezimungu mwingi wa rehema kutujaalia leo tukakutana hapa. Mhe. Mwenyekiti, kama ulivyosema kwamba leo muda ni mdogo na ni kweli ni mdogo lakini nataka niende mbio mbio ili niweze kuchangia.

Mhe. Mwenyekiti, la kwanza ninalotaka kulizungumza ni suala zima la kilimo hasa cha mikarafuu. Mhe. Mwenyekiti, kilimo cha mikarafuu kama tulivyoona kwamba wizara imeweza kufanikiwa kwa kiasi kikubwa kuongeza uzalishaji wa zao la karafuu kama ilivyosomwa kwenye bajeti ya Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda. Ni dalili tosha kwamba zao la karafuu kwa sasa toka zamani ni tegemeo lakini kwa sasa limezidi kuwa tegemeo na uzalishaji wake umeongezeka naipongeza serkali sana kwa kuliona hilo.

Lakini pia nilikuwa napenda kutoa ushauri mmoja na ninaishauri wizara miongoni mwa jambo muhimu ambalo litatusaidia moja ni kuweka malengo katika uzalishaji, tumefikia tani elfu nane na mia tano lakini tuwekeni lengo tuweze kujua kama lengo letu ni kufikia mfano tani 15,000. Kupitia kwa wataalamu wetu nawaomba sana Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, kutumia wataalamu wafanye tathmini waweze kutupa tathmini hizi tani 15,000 za karafuu tunaweza kuzipata kwenye miti mingapi. Mhe. Mwenyekiti, ili tutakapokwenda katika malengo tujue tunakwenda wapi, tukishakujua idadi ya tani 15,000 kwa muda angalau wa miaka 10 tutakazoweza kuzizalisha. Vile vile tuweze kugawa miche kwa mujibu wa lengo la tani 15,000.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, leo hii mimi kidogo nilikuwa linanipa wasi wasi kidogo na ninaiomba serikali isikilize kidogo maoni yetu na najua ipo serikali yetu tukufu, sikivu kwamba tunagawa miche mingi ya mikarafuu inayotolewa. Naipongeza serikali kwa kugawa miche hii kuwapa wakulima wa mikarafuu bure, lakini uendelezaji wake unakuwa ni hafifu.

Mhe. Mwenyekiti, leo lau kama tungelikuwa miche ile tunayoitoa inatunzwa na inaendelezwa kama ilivyo. Imani yangu ni kwamba leo kwa Pemba na Unguja tungekuwa hatuna tena sehemu ya kupanda mikarafuu. Ninashauri kwamba bora tuzalishe kidogo tuigawe kidogo miche ile ya mikarafuu, lakini tuhakikishe inakua ili iweze kufikia lengo la kuzaa na hatimae kuweza kusaidia ukuaji wa uchumi kwa taifa.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu gani, hadi leo mikarafuu tuliyokuwa tunaichuma ni mikarafuu ambayo tumeirithi kutoka kwa wazazi wetu mingi, penginepo asilimia 30 au chini ya asilimi 30 ndio mikarafuu inayotegemewa kuzaa kuanzia kipindi cha ndani, kuanzia mwaka pengine 2015, 2016 baada ya serikali kuanza kuigawa hii miche. Kwa hivyo hilo naiomba sana serikali na natoa nasaha kwa wakulima wenzangu ile miche ambayo tunapewa, ile miche ambayo serikali

inatoa tuweze kuitunza, kuiendeleza ili ifikie lengo la kuzaa na hatimae kupata ile faida tulioikusudia. Haitakuwa jambo la busara kufika msimu tukachukua miche ya mikarafuu tukenda tukaipeleka mashambani baadae tukaitupa au serikali imetoa miche ikisha baadae mkulima yule yule asubiri tena serikali ikamsaidie kuitunza.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo napenda niende kwenye kilimo cha mpunga. Ninapenda kuipongeza sana serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa kuongeza kilimo cha mpunga. Zao la mpunga limeongezeka lakini kwa mwaka jana tulikuwa na matatizo kidogo wakulima walipata matatizo ya kuchelewa kwa matrekta, lakini kwa sasa matrekata yale yapo nimeyaona, hongeza sana Mhe. Waziri kwa kutuletea matrekta mapya. Lakini kwa kwetu pia kwa msimu wa mwakani wa 2019/2020 tutakapoingia, tujitahidi katika mabonde yale yaliyopo Konde hasa na baadhi ya mabonde ambayo nayajua yapo katika Jimbo la Mtambwe yaweze kufika, kule kuna mabonde mara hii hayakupata kulimwa kwa trekta kwa sababu ya uchelewaji huo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia niende katika suala zima la uvuvi. Suala la uvuvi sasa hivi tumekuwa na tatizo kubwa la uharibifu wa mazingira hasa kwa upande wa matumbawe. Mhe. Mwenyekiti, kama tunavyoamini na tunavyojuwa kwamba ndio mazalia ya samaki, lakini sasa matumbawe yale yameanza kupotea kwa kiasi kikubwa. Hii inatokana na baadhi ya wavuvi wetu kwamba hawapo na ile, tuseme mfano tamaa imewazidi, haiwezekani kwamba mtu kwenda kuvunja mpaka yale mazalia ya samaki, unategemea nini. Nitoe wito kwa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwamba iko haja sasa ya kuanzisha *patrol* ya baharini ili kuweza kuwabaini wale wavuvi ambao wanayaharibu yale mazalia ya samaki na ambao wanavua samaki wachanga ukiachilia mbali wale samaki ambao ni wadogo toka asili maumbile yao.

Mhe. Mwenyekiti, leo hii kama yuko mwezangu mchangiaji mmoja alizungumza kwamba unaweza kwenda sokoni ukawakuta samaki, unamkuta changu kweli changu lakini samaki mdogo mno ambaye ungeweza kumuacha kwa maalum angalau ungeweza kusaidia. Leo tumekuta baadhi ya wavuvi ambao wameweza kuhifadhi maeneo yao, wakati niliponikitembelea maeneo ya Kizimkazi tulipewa hiyo habari kwamba watu wamehifadhi maeneo yao ya uvuvi wa pweza, leo ikifika kipindi wanaweza kuvua pweza wengi.

Mimi nichukue fursa hii kuwapongeza sana na nawaomba sana wavuvi wengine wafuate ule utaratibu wa kuyahifadhi, kwa sababu yale maeneo ni yao. Lakini pia na Wizara nao kupitia Idara ya Uvuvi, niwaombe tu na niwatake kwamba waende

vijijini kwa wavuvi wetu wakatoe taaluma jinsi ya kuhifadhi yale maeneo ili wavuvi waweze kujua faida ambayo wanaweza kuipata iwapo wataweza kuyahifadhi yale maeneo yao.

Mhe. Mweneyekit, kwa sababu yale maeneo ni yao, samaki ni wao baada ya muda watavua wao wenyewe. Ni juu tu ya wao wenyewe kuweza kujizuia kwa muda maalum baadae wakaweza kuvuna wakapata mazao ambayo yatawaleta kipato zaidi. Lakini wavuvi wetu kama tunavyowafahamu ni watu wanaohitaji kupewa taaluma. Niombe sana wizara kupitia Idara ya Uvuvi jambo hili waliangalie la kuweza kuwashajihisha wakulima wetu waweze kuhifadhi maeneo ya uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho napenda nichaangie kuhusu suala la ufugaji kwa upande wa ufugaji tumekutia kuna wimbi sasa ambalo limejitokeza la wizi wa mazao na mifugo, wimbi la wizi wa mifugo kwa Zanzibar sasa hivi kwa Unguja na Pemba limekuwa ni tatizo. Wafugaji leo mtu haina imani hata ya kufuga kuku wale kuku wa kienyeji mitaani kila unapopita watu wanalalamika kuku wameibiwa, kuku wanafanya hivi. Niombe sana tu Wizara ya Kilimo kupitia Idara yake ya Mifugo kwamba ifuatilie karibu na iwe karibu na Masheha ianzishe utaratibu wa takwimu ya mifugo ili waweze kujua wafugaji wa asili, waweze kuwatambua pia wafugaji wa kisasa.

Jambo hili litapunguza sana wizi wa mifugo na vile vile kama lilivyozungumzwa jana katika suala la msingi na Mheshimiwa kwamba wananchi wa maeneo mengi yeye aliyataja baadhi ya maeneo wanalalamikia tatizo hili la wizi wa mifugo. Hebu Mhe. Waziri utakapokuja uniambie katika jibu lako umejipanga vipi kukabiliana na hili tatizo la wizi wa mifugo hasa ambalo limekithiri na linawanyogonesha hasa wafugaji wetu. Hili ni chukizo mfano katika jimbo langu kabla ya Ramadhani mwezi wa Shaaban huu kuna taarifa niliyoipata kuna kijiji kimoja siku moja waliibiwa ng'ombe wane, tufikirieni hebu mtu huyu anakuwa kwenye hali gani. Mheshimiwa tatizo la wizi wa mifugo nakuomba sana ulichukulie na ulitilie mkazo kwa aina yake tusije...

Mhe. Mwenyekiti: Muda wako umemaliza

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, napenda kuunga mkono hotuba hii asilimia mia ahsante sana.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante pia kwa mchangio wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Miraji Khamis Mussa na akifuatiwa na Mhe. Shaib Said Ali ajitayarishe.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa nafasi ya kuchangia Hotuba ya Makadiri ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijaenda katika michango yangu naomba niseme wazi nia ya kuzuwia mafungu matatu ambayo fungu la Programu ya Raslimali ya Misitu, Maliasili Isiyorejesheka lakini Programu nyengine ya Utawala na Uendeshaji wa Kazi za Kamati, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ambapo kuna Programu ndogo ya Uratibu wa Kazi za Wizara Pemba, lakini Programu ya

mwisho ambayo nina nia nayo kuzuwia fungu ni Programu ya Utawala wa Kazi za Kilimo, Maliasili na Mifugo. Naomba niende kwenye michango yangu baada ya kutoa nia yangu ya kuzuia fungu kwenye maeneo haya.

Mhe. Mwenyekiti, mchango wangu naomba nianzie kwenye Programu ya Mipango ya Uendeshaji wa Kazi za Kilimo. Mhe. Mwenyekiti, katika eneo hili nimepitia kitabu vizuri lakini katika kitabu kilichopita walitueleza na wakatupa taarifa kuwa kuna mapitio ya Sera ya Kilimo, walifanya kazi mapitio ya Rasimu ya Sera ya Kilimo ya mwaka 2002 ambayo sera hiyo imefanyika pamoja na kuchukua maoni ya wadau mbali mbali Unguja na Pemba. Sasa nilikuwa nataka kujua Waziri atakapokuja kwa sababu tuna wasi wasi au mashaka fulani kuwa wizara inakwenda bila ya sera, kwa sababu walisema wamefanya mapitio ya Rasimu ya Sera ya Kilimo ya mwaka 2002. Mapitio yale wameshakamilisha kwa sababu walikuwa na rasimu wameshakuwa na sera kamili mpaka muda huu tuliokuwa nao sasa na kama hawana ndio dhamira yangu ambayo nataka kuzuwia fungu.

Lakini eneo jengine walisema kuwa wamefanya utafiti wa kujua uwezo wa uzalishaji wa mazao ya embe, machungwa, na nazi lengo kubwa ni kuboresha eneo hili na kuingia katika soko ambalo litaweza kusaidia kukuza pato maana yake la serikali. Sasa nilikuwa nataka kujua ule utafiti uliofanyika mafanikio yake maana hayakuelezwa katika kitabu hiki ambacho tumekipokea hivi sasa hivi. Kwa hivyo sasa tunataka kujua kwa sababu tunafuatilia cha mwaka 2016/2017 na 2017/2018. Sasa wakieleza kule mafanikio wanayo wanayopata wakishindwa kutuambia huku tunapata mashaka. Isije kuwa kila siku tunapewa ripoti lakini ule utekelezaji wake baadae unaishia kati tunapewa mengine, sasa nidio maana nikasema eneo hili nina dhamira ya kuzuwia fungu.

Lakini niende tu haraka hara kwa sababu nina dakika kumi hizi zinaweza kunishia njiani yale mambo mengi sijayataja kuna eneo la Programu ndogo Pemba katika utawala nilisema nimshukuru kwanza waziri, niwashukuru sana watendeaji kuwa wameeleza vizuri mapato mengi yaliopatikana kwenye mchanga wameeleza lakini wameacha kutuambia kunako eneo la ukodishaji wa mashamba ya karafuu wamepata kiasi gani, lakini kama waliingia mikataba na watu kimebaki kiasi gani. Kwa hivyo katika eneo hili tunataka taarifa kamili za mwaka huu wa fedha katika ule ukodishaji kilichopatikana na kinachosubiriwa kwa sababu tunaingia mikataba na watu sasa maeneo yamenda vizuri.(*Makofi*)

Lakini eneo la Programu ya Rasilimani Misitu hapa Mhe. Waziri kuna maeneo matatu ambayo nataka kuyachangia. Eneo la mwanzo Mhe. Mwenyekiti, ninalotaka kuchangia ulisema kuna ongezeko la uchimbaji wa mawe, kifusi na mchanga. Lakini katika eneo hili la mawe na kifusi kuna maeneo mengi tuliachiwa na tuliruhusu na tukatoa vibali kama Jumbi, Kandwe, Kisauni, Matemwe haya yote mpaka sasa hivi hatujaona ule mpango wa serikali kuyarejesha. Maeneo ya mchanga nitayazungumizia baadaye lakini nianze katika maeneo haya. Sasa nilikuwa nataka utakapokuja tujue ule mkakati wa serikali huwa tunakwenda ni faida kwetu tunapata kipato, lakini tusipoyaresha maeneo yale ni hatari ndani yake. Nilikuwa kujua ule mkakati wa serikali ndio maana nikasema hapa nijue serikali ina mpango gani wa kurejesha katika maeneo yale.

Lakini niende kwenye mchanga. Katika eneo la mchanga huku ndio kuna ongezeko kubwa la mazingira yetu ule uchafuzi wa mazingira yetu mchanga ni raslimali moja ambayo inatuingizia kipato tunapata kujenga. Lakini upo mpango wa serikali kurejesha ardhini, ndani yake tunapochimba mchanga kuna asilimia inakwenda katika kufidia kurejesha kwa ardhi ile ambayo hii inakwenda katika Idara ya Mazingira. Sasa nilikuwa nataka kujua katika mwaka huu wa fedha kiasi gani kimekwenda kuchangia katika mfuko ule wa urejeshaji wa ardhi ambayo imechimbwa mchanga ambayo Idara ya Mazingira utakapokuja katika bajeti yao ya Wizara ya Ardhi nayo na *declare* kuchangia Mwenyezi Mungu akijalia naweza kuzuwia fungu la eneo hili ili kupata taarifa za kilimo na watu wa ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini eneo hilo hilo la mchanga pia kuna mkataba hapa ambao serikali imeingia na yule ambaye anapakia ule mchanga wenyewe kwa magari mbali mbali. Ndani ya mkataba huo kuna tani ambayo tumeiweka wenyewe ya kuzisaidia jumuiya mbili, kwa kila tani shilingi mia. Lakini mpaka leo hii kadhia wizara yako haijatufikisha pahapa pazuri, kwa sababu kuna eneo kubwa na la watu wengi ambao wanasubiri huduma hii, ili wapate kufanya yale ambayo yamekusudia kupitia jumuiya zao. Maana kuna Jumuiya ya Upakizi na Utunzaji wa Mazingira lakini kuna Jumuiya ya Wamiliki wa Magari yanayosafirisha huo mchanga wenyewe. Sasa ukija Mhe. Waziri unambie wizara yako imekwama nini kwenye jambo ambalo mumeshakubaliana katika utaratibu ambao mlisema mtawachangia hawa ili kuondoa zile tofauti zilizokuwa zinatokezea muda wote ambao kazi hii kule Donge ikiwa inafanyika.

Mhe. Mwenyekiti, nende pia katika kadhia nyengine ya uchimbiji wa mchanga kwanza hapa nimpongeze sha Mkurugenzi wa Misitu pamoja na wasaidizi wake, na naomba kumpongeza kwa sababu amefanya kazi zake vizuri maeneo haya yote. Lakini tunataka kujua kuna hoteli ilikuwa inajengwa Maruhubi na nikieleza maeleza yangu sina haja ya kuitaja walifukia ardhi maana walichimba mchanga wakafukia ardhi, lakini kuna mchanga mwengine ukatoka eneo moja ukawa unapelekwa eneo jengine Fumba. Yapo magari sisi tuna taarifa yalizuwiwa. Kwa hivyo tunataka kujua hatua ambayo Mkurugenzi kenda vizuri, lakini pale mwanzo mpaka anachimba ile ardhi yenyewe anafukia kuna *study* gani ambayo imefanyika, kwa sababu jambo kubwa kama lile sisi tunalipongeza, lakini adhari zake wakati fulani zinakuwa nyingi.

Sasa hivi ikifika mwezi kumi na tano maji yanapanda sana, yanakwenda kuathiri nyumba za watu wetu au wananchi wetu, lakini ikifika mwezi ishirini na tisa au thelathini pia athari hiyo inawakumba watu wetu kila leo hapa tunapozunguza. Sasa lazima serikali inapotaka kufanya jambo mimi naamini hata katika uwekezaji mkubwa unafanya *feasibility study,* kwa sababu nilikuwa nataka kujua na watu wa mazingira nawasubiri lakini kwako wewe Mhe. Waziri unalotakiwa unijibu ule uondoaji wa mchanga kulikuwa na makubaliano gani kutoka eneo moja kwenda eneo jengine na kama hayapo kwa nini vifanyike vitendo kama hivyo lakini serikali imechukua hatua gani.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende kwa wakulima. Mhe. Waziri katika hotuba yake nimpongeze sana amejaribu kutuonesha dhamira ya serikali kuleta matrekta yaliopo, pembejeo lakini niwe mkweli miongoni mwa hao wakulima na mimi nimo, hawa watu ambao tunawaita mabwana shamba, mabibi shamba au wataalamu wetu katika eneo hili la kilimo Mhe. Waziri hawafikii wakulima, hawafikii kabisa. Leo hii katika bonde kama la Upenja kunako kilimo lakini kunako

vilimo vyengine unaweza ukatafutana naye wataalamu hawa ili wakupe tu ule ushauri wa kitaalamu ili lile ongezeko la mazao yetu lile linafanyika vizuri tukutane nao. Sasa nilikuwa nataka kujua labda tunawasubirie wapi. maana wao walipaswa kuwatafuta wakulima wenyewe lakini na wakulima wanapaswa kuwatafuta wataalamu wenyewe, lakini katika sura ya kawaida unaweza ukiende Kilombero hukutani naye, unaweza kwenda Kibokwa hukutani naye...
Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa una dakika moja malizia.

Mhe. Omar Seif Abeid: Dakika moja eeh! Mhe. Mwenyekiti, dakika yangu moja naomba kuunga mkono kwa asilima hamsini, hamsini nabakisha na yale ambayo sijachangia nitapeleka kwa maandishi lakini nia yangu ya kuzuwia mafungu ipo pale pale. Jambo kubwa ambalo nimekuwa nimebakisha ilikuwa ni sehemu moja ya uvuvi katika dhamira ile ya kununua meli lakini hilo nitamuandia Mhe. Waziri kwa maandishi ili tuweze kupata majibu yanayostahiki.

Ahsante nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mraji. Sasa naomba nimwite Mhe. Shaib Said Ali na baadae Mhe. Panya Ali Abdalla ajitayarishe.

Mhe. Shaib Said Ali: *Bismillah Rahman Rahim.* Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote kwanza nikushukuru wewe kabisa kunipatia nafasi hii lakini la pili nimshukuru Waziri na Naibu Waziri. Naibu msomi na Waziri mfanyakazi kwa kupewa Wizara hii mbayo ni wizara mama katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa vile muda ni mdogo nianze mchango wangu katika wizara yake ukurasa wa 47 kifungu (D). Nikisome kidogo, "Ulipaji wa fidia ya mazao kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji Zanzibar katika mabonde ya Mwanakwereke na Mlemele kwa Pemba". Mheshimiwa nipo hapa katika bonde la Mlemele.

Mheshimiwa bonde hili sijui Mhe. Waziri hii miundo mbinu anakuja iweka wapi. Namuomba Mhe. Waziri anifahamishe hii fidia na miundo mbinu anawalipa nani ambayo hilo bonde sasa hivi huu ni mwaka usiopungua ishirini na tano ninavyokumbuka mimi, bonde hili limo katika bajeti lakini linamalizia katika vitabu hivi. Sasa mimi nimuombe Mhe. Waziri leo anieleze hapa hili bonde hasa linaendelezwa nini katika ukulima huu wa umwagiliaji maji na kama mheshimiwa haliwezekana basi wale wananchi wangu watolewe hii taama.

Mhe. Mwenyekiti, tamaa ikiwa kubwa mheshimiwa mbaya kumuweka mtu miaka ishirini na tano vibaya sana wamtia tamaa tu nitakufanyia kesho, keshokutwa, mtondogoo na kavu. Sasa kama hili wanaona haliwezekani kumwagiliwa maji kufanywa katika bonde la umwagiliaji maji wananchi wangu waambiwe, huu ni mwaka wa ishirini na tano mheshimiwa na hivi sasa limo katika bajeti kama watalipwa wananchi fidia na miundo mbinu. Bonde la Mlemele sijui hiyo miundo mbinu iko wapi. Kwa hivyo Mhe. Waziri nakuomba kwa dhati kabisa unielezee vipi bonde hili litakuwa la umwagiliaji maji. Bajeti ya 2017/2018 tuliambiwa kuwa bonde hili tayari limeshaingizwa katika kila suala na litafanyikwa kazi na fedha ikapangwa, lakini Mheshimiwa sijui kama lilipitiwa bonde hili. Kwa hivyo nimwambie Mhe. Waziri kama haliwezekani hawa

wananchi wangu nasema tena waondoshe tamaa ya kuambiwa kwamba lile bonde la Mlemele litakuwa bonde la umwagiliaji maji katika visiwa vya Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo nije katika programu ndogo ya kilimo ukurasa wa 50 kifungu cha 73 suala zima la mbegu na dawa kwa wakulima. Mheshimiwa hapa pana kilio hususan dawa za kuulia magugu. Mheshimiwa bado nakuomba tufanye utafiti hawa wananchi wapate dawa za kuulia magugu, hicho hicho kilimo cha kijembe mkongoroka bado wananchi wanakitumia lakini dawa za kuulia magugu zinawashinda vipande vyao vinaharibika mheshimiwa, kwa sababu watu wetu na mbolea, mheshimiwa watu wetu wanachoka kuinama kupalilia sana. Tunaomba hizi dawa zipatikane mheshimiwa, wanawake wanapata tabu katika masuala haya. Mheshimiwa mwanamke anainama kuanzia saa moja asubuhi mpaka saa tisa, akija kwake anafanya kitu gani mwanamke kama huyo. Mheshimiwa tunaomba kabisa kwa dhati kabisa kwamba hizi dawa wafanye utafiti ni kiasi gani cha dawa zitakazopatikana. Lakini la kushangaza Mheshimiwa dawa hizi hizi lakini badala yake madukani unazikuta zinauzwa kwa shilingi thelathini na tano mpaka arubaini kwa nini. Mhe. Waziri naokuomba ufanye utafiti.

Mhe. Waziri nakuhakikishi kwamba safari hii Sheha wangu wa Pujini alipigwa kwa dawa hizi, hakujua vipi azigawe wananchi wakamvamia na kumpiga. Kwa hivyo nakuomba Mheshimiwa nakuomba sana kama hizi dawa hazipatinani, vile vile nasema kwamba lakini kama zitapatikana basi zipatikane kwa wingi.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapa niende katika suala la matrekta. Mhe. Waziri safari hii kilimo kwa uwezo wa Allah namini kwamba kitakuwa kizuri na kwa vile matrekta yameshaingia namini kwamba nashukuru sana kwamba kitaendelea kuwa kizuri zaidi. Lakini Mhe. Waziri namuomba anieleze hii trekta inalima kilimo cha yale mashamba ya mpangilio tu au kwa wananchi wote mpaka yale mashamba yalikuwa hayamo kwa mpangilio. Kwa sababu Mheshimiwa mashamba yaliyokuwa hayamo katika mpangalio, haya matrekta yanalima kwa bei kubwa sana. Sasa mimi namuomba Mhe. Waziri akija hapa anieleze haya mashamba yaliyokuwa hayamo katika mpangilio bei yake ni yapi lakini mashamba yaliomo katika mpangilio bei yake ni ipi. Mheshimiwa hapa pana ujanja mmoja wanaoufanya madereva hususan kule kwetu Pemba. Kuna wakati matrekta huambiwa kwamba sasa hivi yanataka kupasishwa kama kufanyiwa *service.* Mheshimiwa wananchi ndipo hapo wanapoumia, kwa sababu ile *service* inakuja moja kwa moja kwa wananchi, mwananchi ana shamba lake anataka kulima mapema lakini pale eka moja analimiwa kwa shilingi 50,000 mpaka 60,000. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri hapa anielezee hawa waliokuwa hawamo katika mpango hawana bei maalum ya kulimiwa mashamba haya kwa matrekta

Halafu matrekta hayo yaliyoletwa safari hii nashukuru sana serikali yangu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuongeza matrekta. Mheshimiwa wasi wasi wangu mdogo tu kwamba haya matrekta katika mabonde yetu yale ya Pemba yataweza kufanya kazi. Kwa sababu tulipata msaada kama huu wa matrekta kutoka Libya lakini kwa bahati nzuri au mbaya matrekta yale hayakuweza kufanya kazi hata mwaka mmoja. Je, haya si yale yale au kuna mengine ambayo ni mazuri zaidi ya yale. Mimi nataka niwaeleze tu wananchi wangu kwamba matrekta yanayokuja safari hii ni mazuri na yataweza kulima kilimo zaidi na zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu haya kama kuna tafiti ardhi ya masuala mengine kama kule kwetu Pemba hususan jimbo langu la Pujini, Chonga na kadhalika ardhi yake ni ngumu sana. Kwa hivyo inataka matrekta yaliyo mazuri. Nimuombe tu Mhe. Waziri atuelezee haya matrekta yataweza kufanya kazi Pujini, maana tusije tukazungumza hapa kwamba tunaleta matrekta lakini kumbe matrekta yale baada ya siku mbili tunaambiwa kwamba hata vipuri hamna ikawa kazi ni ile ile.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo nije katika masuala ya mabadiliko ya tabianchi. Mhe. Mwenyekiti, namuomba tena hapa Mhe. Waziri tufanye tena utafiti. Kwa sababu Mwenyezi Mungu katujaalia safari hii kutokana na hali ya hewa kuvurugika mazingira kuyachafua, hivi sasa mwananchi hajui ni wakati gani wa kupanda zao gani, wakati gani wa kupanda zao gani. Sasa nimuombe Mheshimiwa kwamba tunabahatisha kupanda mazao yetu na kwa vile Wizara yake ya Kilimo naamini kwamba ni wizara moja ambayo ina wasomi wengi, watafiti wengi, wajuzi wengi, naiomba wizara hii ifanye utafiti irudishe vile vile wakati wa maandalizi ya mpunga ni upandaji wa kunde, wakati wa kupanda kunde tunapanda kitu gani na kadhalika, ili wananchi wapate. Mhe. Mwenyekiti, safari ni kwamba wananchi wanajipandia tu mazao ni kwamba hawafuati tena ile miongo, ile miongo yao imewapita. Kwa hivyo Mhe. Waziri namuomba hili suala aliendeleze zaidi ili wananchi wapate kunufaika katika ukulima wao mzuri.

Mhe. Mwenyekiti, halafu nije katika usimamizi wa mali zisizorejesheka. Mheshimiwa hapa tuliambiwa kwamba serikali ina nia ya kupanda miti katika maeneo yale. Hivi sasa niseme kwamba eneo kubwa la ukanda wa mashariki katika Kisiwa cha Pemba, karibu kutakuwa hakufanyiki tena kitu kwa sababu ni kwamba kuna mashimo mengi sana ambayo hivi sasa yanaleta hatari. Nimuombe Mhe. Waziri suala la upandaji wa miti liingizwe kabisa, kwanza namuomba yale mashimo yafukiwe halafu ndio papandwe miti. Kwa sababu bila ya kufukia yale mashimo itakuwa bado hakujakuwa na suala zima la uboreshaji wa hii raslimali ambayo hairejesheki.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo nije katika sehemu ya huduma za utibabu wa mifugo. Mheshimiwa bado wataalamu wake wa utibabu wa mifugo hawajapitia vijijini kwenye mifugo. Vijijini mifugo inapotea kwa wingi kama utakuwa na takwimu nzuri, kama utakuwa na hesabu nzuri, kama utakuwa na ufuatiliaji mzuri, basi niseme kwamba ndani ya vijiji vyetu wanyama wanakufa kwa wingi wakati hawana matibabu mazuri. Nimuombe Mhe. Waziri afanye tena utafiti wa matibabu ya wanyama ili wanyama wetu wapate neema kwa sababu hapa baada ya kilimo mwananchi hutegemea sana mifugo yake, lakini leo kuna bwana ng'ombe wale na bwana kuku, lakini leo ukimwendea mtu yule anakwamba mimi sina dawa, sina usafiri, sina chochote umuhudumie kwa kila kitu ili aje akutibie wanyama wako. Nimuombe Mhe. Waziri kwa huruma zangu na unyenyekevu wangu bado suala hili ni gumu katika vijiji vyetu. Kwa hivyo uwape vipando wale mabwana ng'ombe na kuku ili watibu wanyama wetu kwa vizuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nisichukue muda wako mrefu kwa sababu naona umeshaanza kuniangalia, najua kwamba muda wangu umemalizika ushaanza kuniangalia. Mimi niunge mkono wizara hii na nimpongeze Waziri, Naibu Waziri, lakini Mhe. Waziri nasema tena kwamba anipe maelezo rasmi. Sina nia ya kupiga buti lakini namuomba anipe maelezo rasmi kuhusu bonde langu la Mlemele.

Naunga mkono hoja Inshaallah Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mwakilishi. Sasa naomba nimwite Mhe. Panya Ali Abdalla na baadae Mhe. Amina Iddi Mabrouk ajitayarishe.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Mwenyekiti ahsante sana, nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu (*S.W)* ambaye ametujaalia uhai tukaweza kukutana hapa. Pia nichukue fursa hii kukushukuru na wewe kuweza kunipa nafasi hii nikaweza kusema machache.

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijaendelea naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Waziri, Naibu Waziri na watendaji wao wote, lakini pia naishukuru na naipongeza sana kamati kwa kazi kubwa na nzuri. Lakini pia nampongeza muwasilishaji wa ripoti hii.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kuendelea niseme kama kilimo ndio uti wa mgongo wetu. Mheshimiwa ili kufanikiwa katika suala zima ambalo tunalitarajia la uanzishwaji wa viwanda basi ni lazima tuwahamasishe wakulima katika uzalishaji. Lazima wakulima wetu sasa wajikite katika kuzalisha miti hii ya matunda, kupanda sana miti hii lakini pia kuzalisha bidhaa mbali mbali ambazo zitaweza kwenda katika viwanda mfano nyanya na kadhalika. Kwa hivyo mimi nianze mchango wangu huu katika suala zima la kilimo cha umwagiliaji maji. Mhe. Mwenyekiti, katika programu hii Mhe. Waziri ametueleza kama katika mwaka uliopita kilimo cha juu yaani kinachotegemea mvua kiliweza kulimwa ekari 26,891. Lakini kilimo kile tunachotegemea cha umwagiliaji kimeweza kulimwa ekari 2,126.4.

Mhe. Mwenyekiti, niseme bado kabisa ile dhamira tunayoitegemea katika suala zima la kuwa na uhakika wa chakula bado hatujaweza kulifikia. Mhe. Mwenyekiti, mnamo mwaka 2011 tulipitisha Sheria ya Usalama wa Chakula Zanzibar. Sheria hii ni Sheria Nam. 5 ambayo imeweka wazi uanzishwaji wa kuhifadhi chakula kwa lengo la kuepusha upungufu wa chakula Zanzibar wakati wa ukame au dharura yoyote itakayotokea kwa lengo la kutatua matatizo yanayotokana na usambazaji wa chakula.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naiomba sana serikali yangu ili tuweze kufanikiwa lazima tujikite katika kilimo cha umwagiliaji ndicho ambacho kitatuwezesha sisi kuweza kufikia kuwa na uhakika wa chakula. Mhe. Mwenyekiti, tunaelewa kilimo cha umwagiliaji mwaka mmoja tunaweza tukalima mara tatu. Kwa hivyo tunao uwezo wa kuzalisha chakula kingi wakulima wetu wakaweza kupata cha matumizi lakini hata wakaweza kuuza na hata chakula cha hakiba kikaweza kuwepo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilitegemea hizi ekari ishirini na sita zingebadilika zikawa ni ekari za umwagiliaji kuliko hivi zilivyo katika ukulima wa kutegemea mvua. Kilimo cha umwagiliaji kingeweza kutufanya sisi tuweze kuwa na chakula chenye uhakika ambacho tungeweza kuzalisha kwa wingi na hasa pale tutakapowapa wakulima wetu elimu ya kilimo hicho. Mhe. Mwenyekiti, naomba sana serikali hili liwe kama jambo la dharura, tulipokuwa tumepata dharura katika suala zima la meli tuliweza kupanga mkakati na tukaweza kupata meli ile kwa ajili ya kutuokoa katika shida zetu. Hili lazima serikali tujipange ili tuweze kuwa na chakula uhakika, kwa sababu tunaweza tukaja tukapata tatizo tukaja tukashindwa kuwa na akiba katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, niseme nataka kujua haya maghala ambayo yametengezwa tumeweza kupata maghala mangapi ambayo yapo, lakini na maghala hayo yanawezaje kufanya kazi mkakati gani serikali imeweza kupanga katika maghala hayo ambayo tumekusudia kuweka chakula ili kuweza kuona tuna chakula cha uhakika.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika utoaji wa miche. Kwanza nichukue fursa hii kuipongeza sana serikali kwa kazi kubwa na nzuri ambayo inaifanya kwa kuwapatia wakulima miche ya mikarafuu na miche mengine. Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema serikali inaendelea kutumia fedha nyingi katika kuwekeza. Sasa kama hatukujipanga vizuri katika ufuatiliaji tunaweza tukaona fedha zinatoka lakini hazifikii yale malengo ambayo tumejipangia. Mimi nilitaka kujua tu serikali inajipanga vipi pale inapotoa miche kwa kumpa mkulima na baadae inafuatiliaje kuona mkulima huyu miche ile ni kweli ameipanda na mingapi imepona na mingapi imekufa, ili tukaweza kuona tunazilinda zile fedha za serikali.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, mimi niseme kuna habari nyepesi nyepesi wala si nyepesi ni nzito kwa sababu serikali yangu inaumia katika kutoa fedha kwamba miche hii tunayoitoa inachukuliwa, serikali inatoa bure lakini miche hii watu wanaiuza na inasafirishwa inakwenda kupandwa sehemu nyengine. Hilo sio lengo la serikali, lengo la serikali wananchi wa nchi hii wafaidike. Kwa hivyo naomba sana serikali inapotoa miche hii ifuatiliwe ijulikane nani amepewa na amepanda na ifuatiliwe na wataalamu hasa iweze kupandwa kitaalamu ili tuweze kuwa na mikarafuu iliyo bora.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu huu niende katika Wakala wa Matrekta. Naipongeza serikali kwa dhati kwa kuona imefanya juhudi ya kutuongezea matrekta haya lakini na yale ya zamani ambayo tunayo imefanya juhudi ya kuyatengeneza. Mhe. Mwenyekiti, mimi ombi langu katika eneo hili nilikuwa naomba Wakala huyu wa Matrekta basi aweze kupatiwa *vote* yake. Ili Wakala huyu aweze kufanya kazi zake vizuri na aweze kumtayarisha mkulima kama hana *vote* ana pesa tu za kusubiri subiri anaweza kushindwa kufanya kazi kwa ajili ya kuwatayarisha wakulima. Mhe. Mwenyekiti, mimi naiomba sana serikali ili tuweze kufikia katika lengo letu ambalo tumelikusudia, basi lazima tuweze kuyafuatilia yale yote ambayo tumejipangia ili tuweze kuyaona yako katika ufanisi mzuri.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache mimi niseme naunga mkono kwa asilimia mia moja hotuba hii ya Mhe. Waziri na namtakia kila la kheri, lakini napenda yale mawazo wanayoyatoa Wawakilishi ambayo yana msingi wa kufanikisha basi yaweze kufaniwa kazi. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mwakilishi. Sasa Mhe. Waziri naona yupo naomba nimpe achangie.

Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii kwanza kabisa kuwapongeza wenzangu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi. Mhe. Rashid Ali Juma na Naibu Waziri na watendaji wote wa wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya kuhakikisha kwamba Zanzibar inaendelea katika sekta hii ya kilimo.(*Makofi*)

Pia naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza kwa kitabu chao kizuri chenye mipango inayotekelezeka, chenye malengo ambayo yako wazi na yanayotekelezeka. Mhe. Mwenyekiti, mimi katika mchango wangu nitazungumzia zaidi mambo mawili, katika Sekta ya Kilimo na Sekta ya Uvuvi. Kwanza kabisa Mhe. Mwenyekiti, ningeomba kidogo niseme kwamba hali tuliyokuwanayo nchi zetu za Kiafrika hata Zanzibar ni hali ambayo nchi zote za Kiafrika inayo, kwa sababu kuna dhana potofu katika sekta ya kilimo. Dhana potofu ni ipi.

Mhe. Mwenyekiti, watu wanaonekana kwamba kilimo ni sawa sawa na kuwa maskini na hili limezungumzwa hata kwenye vikao vya juu vya Umoja wa Mataifa, vikao vya Umoja wa Afrika, na vikao vyengine vya nchi mbali mbali, kwamba vijana hawaingii kwenye hii sekta ya kilimo kwa sababu wengi wao hawaoni tija yake kwa vile hawaoni kwamba kuna watu wameweza kuwa matajiri, wameweza kuwa viongozi wa mfano katika sekta hii kutokana na sekta hii ya kilimo. Kwa hivyo wakati umefika wa kubadilisha dhana hii potofu, sekta ya kilimo ni sekta inayowezesha mtu akawa tajiri, akaweza kuwa kiongozi wa mfano katika jamii yake. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, jana Mhe. Suleiman alituuliza katika mchango wa Wizara ya Biashara na Viwanda, kwamba kuna mwelekeo gani sisi kama watu wa Wizara ya Biashara na Viwanda. Sera iliyokuwepo hapa Zanzibar ambayo inatumika nchi nyingi za Kiafrika ni sera ya kuondosha umaskini na Tanzania imepiga hatua kubwa kuondosha umaskini. Takwimu zinatwambia *level* ya umaskini kabisa imepungua sana. Kwa hivyo tumeshapiga hatua nzuri ya kuondosha umaskini, lakini kuna haja sasa ya kwenda mbele zaidi ya hapo na kuwafanya watu wawe na uwezo mkubwa wa kuweza kujiendeleza, wa kuweza wao kuwaajiri wengine, wa kuweza wao kufanya viwanda.

Mhe. Mwenyekiti, lakini tusijidanganye kwa nchi za Kiafrika uwezo huo unatokana katika sekta ya kilimo peka yake na uvuvi. Kwa hivyo ninachotaka kusema kwamba lazima tuongeze uwezo kwa vijana wetu, uwezo wa kuwa na fedha za kutosha za kujikimu wao kimaisha. Kwanza kusimamisha umasikini lakini nyengine za kujikimu kimaisha na kuweza kufanya *investment* ambazo zitasaidia kujenga taifa. Huwezi kufanya hivyo Mhe. Mwenyekit, bila ya kuangalia mambo matatu muhimu.

Lwa kwanza teknolojia lazima ibadilike iendane sawa na wakati huu na kwa sekta ya kilimo lazima tuangalie suala zima la teknolojia itakayowawezesha vijana wetu waweze kufanya kazi ya kilimo. Vijana wetu ukiwaambia waweze kununua vifaa vikubwa matrekta na vyenginevyo watategemea mpaka siku za mbele serikali iwapatie. Lakini kuna zana mpya za sasa hivi za kuwawezesha kufanya kazi za kilimo kwa urahisi, tuangalie basi tutawawezeshaje vijana wetu waende katika teknolojia ya kisasa itakayowawezesha kufanya kazi kwa urahisi wakapata faida.

Mhe. Mwenyekiti, jengine lazima tuangalie mikakati mipya hasa kwa Zanzibar. Tuangalie kilimo hai, najua kilimo hai kina matatizo ni kazi kubwa kwanza kuwapa elimu, kuwafahamisha kuwa na vyombo vya kutoa *certificate* hizo zikubaliwe ni kazi ngumu. Lakini nasema hakuna kilichokuwa rahisi katika dunia hii na ili Zanzibar iendelee tukubali kwamba tujitolee tufanye kazi na tutumie uwezo wetu wote, lakini kazi ngumu zifanywe na wakati wenyewe ndio huu Mhe. Mwenyekiti.

Jengine katika hilo hilo tuangalie utaratibu mzima wa umwagiliaji tusitegemee miradi mikubwa sana ya umwagiliaji ambayo ya kitaifa, lakini pia tuangalie utaratibu gani tutafanya katika suala zima la umwagiliaji ambao utaalamu huo upo. Kwa mfano, masuala ya *drip irrigation* na masuala mengine. Mimi juzi nilikuwa na mama mmoja ambaye ana Kiwanda cha *Plastic* kule Bara, alinambia kwamba India imepiga mapinduzi ya kilimo na mapinduzi ya maziwa na uvuvi kwa kuangalia na kuunganisha sera za fedha, sera za kilimo, sera za uchumi kwa jumla na kuweza kusimamia sekta hii ya kilimo na sekta nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, alinambia hivi, akasema kwamba kwa kule India kila familia ilipewa eka kumi, sisi tuangalie familia zetu tutafanya njia gani za kuwawezesha vijana ndani ya familia zile wapende kilimo na kazi hizi wazifanye. Kwa hivyo utaratibu mzima wa umwagiliaji tuutilie nguvu hasa kwa kutumia zana za kisasa, *drip irrigation* na mambo mengine ambayo utaalamu huo upo tuwawezeshe. Lakini kubwa lazima vyombo vya fedha kwa sasa hivi tushirikiane pamoja ili tuweze kutoa pesa nyingi na kuwasaidia hawa vijana wetu katika sekta hii ya kilimo.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, jengine nataka niseme kwamba lazima tujipange, kwa vipi? Maana yake hatuwezi kulima vitu vyote, hatuwezi kufanya vitu vyote kwa wakati lazima tuone kipi ambacho kitakuwa na maslahi kubwa zaidi kwa vijana wetu na wakulima wetu. Mimi kwa upande wangu niliona na ndio ambalo tutazungumza pamoja na wenzetu wa Wizara ya Kilimo nilitaka wenzangu hapa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza waangalie, kwamba wakati umefika sasa hivi na mimi namuunga mkono Mhe. Panya Ali Abdalla aliyosema twendeni kwenye kilimo cha biashara.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, tumeshafundisha watu wanajua lakini bado nguvu zetu hatujatia katika kilimo cha biashara. Kwa mfano tukizungumza viungo na matunda Mhe. Mwenyekiti, huko ndiko kunakotakiwa viungo, matunda na usarifu wa matunda. Kwa mfano, sisi tunawashukuru sana Wizara ya Kilimo tumepewa viwanda viwili cha Pemba na cha Kizimbani ina maana kwamba hapa tunatakiwa tulime zaidi kama alivyosema Mhe. Panya Ali Abdalla.

Kwa hivyo ninavyokusudia kusema tuone tunatoa kipaumbele vipi kwa kilimo cha viungo. Sasa hivi Mhe. Mwenyekiti, natoa mfano Kaskazini walikuwa wakilima hiliki, tangawizi na vitu vyengine, twendeni huko Wizara ya Kilimo na Ugatuzi sasa hivi na Tawala za Mikoa tushirikiane na sisi sote watatu tuhakikishe kwamba vilimo hivi vinasimamiwa na wanapewa mbegu, wanapewa utaalamu tunawashajihisha watu wa fedha, mabenki nini, wanawasaidia hawa kulima.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, naenda mbio mbio...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa malizia. Naomba umalizie Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda: Namalizia.

Mhe. Mwenyekiti, niseme tu kwamba katika suala la uvuvi wakati umefika sasa hivi tumeshawafundisha watu wengi mambo ya uvuvi, kufuga na nini, na soko lipo Mheshimiwa.

Kwa hivyo sasa hivi tuanze kufanya biashara na vijana waelekezwe kwenye biashara ya kuuza vitu vya uvuvi kwa mfano pweza, majongoo ya pwani na kadhalika. Lakini lazima tuwe na *laboratories* muhimu za kuwapa *certificate* kwa sababu mimi nina watu wa China sasa hivi wanataka kununua hivi. Kwa havyo mambo yote haya Mhe. Mwenyekiti, yanatakiwa tuyasimamie kwa nguvu zetu zote.

La mwisho muhogo. Mhe. Mwenyekiti, hatulimi muhogo sasa, upo muhogo tunakula wenyewe. Lakini muhogo sasa hivi kuna soko kubwa. China juzi wamenambia wanataka muhogo tani milioni moja na hili wenzangu Waheshimiwa katika maeneo yenu tukae na wataalamu wa Wizara ya Kilimo watuelekeze huko.

Baada ya kusema hayo naunga mkono hoja hii ya Mhe. Waziri, Wizara ya Kilimo hawa ni wenzetu wabia katika wizara bila ya kilimo Mheshimiwa sera yetu ya viwanda haitokwenda kwa hatua hatua ambazo tunaitaka iende.

Baada ya kusema hayo naunga mkono bajeti hii. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri. Sasa nimpe nafasi Mhe. Naibu Waziri. Mhe. Naibu Waziri tumia muda vizuri kama dakika 15 ili tuweze kumpa Mhe. Waziri naye kuweza kujibu hoja.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa idhini ya Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi naomba kueleza kama ifuatavyo.

Kwanza, kabisa napenda kuwapongeza sana Waheshimiwa Wawakilishi kwa *concern* yao ya kutaka kilimo hichi kiendelezwe tena kiendelezwe kwa nguvu na kasi yote. Kwa kujumuisha yote waliyoyasema wamesisitiza kama ile msisitizo uliokuwepo wa kuendeleza MTAKULA, yaani tuvue kitaalamu, tulime kitaalamu, tufuge kitaalamu ili tuweze kupata mazao tule tushibe na mengine tuweze kusafirisha nchi za nje kwa ajili ya kupata matumizi mengine ambayo hatuzalishi hapa nchini. Nawapongeza sana kwa hili.

Sasa kwa sababu ya muda naomba moja kwa moja niingie kwenye michangio iliyotolewa na Wajumbe mbali mbali.

Kwanza kabisa nikianza, naanza na michango ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo. Kwa kweli hawa wametupa michango mingi sana na yote tunaipokea na tutaifanyika kazi. Hakuna mchango ambao wameutoa hauna maana yote ina maana. Tunawahakikishia tutazidi kushirikiana nao ili tuendeleze hichi kilimo chetu. Ushauri wa ununuzi wa matrekta ya kutosha waliotupa umeshaanza kufanyiwa kazi na tunategema matrekta haya yatafikia mia ikiwezekana. Ushauri waliotupa wamesema kwamba wakala wa matarekta kutokupangiwa fedha. Nasema kwa mwaka huu 2018/19 wamepatingiwa fedha au ruzuku kutoka serikali bilioni moja pointi tatu saba, kati ya hizo milioni mia sita na arubaini na nne pointi saba ni mishahara na milioni mia saba ishirini na tano ni matumizi mengineyo.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati pia ilituaidhi kwamba hapajatekelezwa kwa ahadi ya kupeleka Makurunge. Sisi tuna hamu sana tuwapeleke Makurunge kwa sababu Makurunge tunajua tumepoteza fedha nyingi za wananchi kupaendeleza, lakini palichwa kwa muda mrefu na sasa tunataka tupaendeleze. Kwa hivyo nawaahidi Waheshimiwa kwamba tutajihidi sana twendwe nayo kamati nzima tukafanye *assessment* kule Makurunge ili waweze kutuaidhi kama wanavyotuaidhi hivi tunavyoendelea.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, pia wamesema hawakuridhishwa na utaratibu wa ugawaji wa pembejeo. Tunasema wizara ilitenga mabonde maalum ya mfano kwa kila wilaya na kutoa asilimia mia ya mahitaji ya pembejeo kwa hayo maeneo ambayo yametengwa maalum. Jumla ya ekari elfu nne mia tano na sitini Unguja na elfu tatu na mia nane na sabini kule Pemba zimeingia katika mpango huo. Mafanikio yaliyopatikana kwa mwaka 2016/2017 wametokana na mpango huo, kiwango cha juu kilichowekwa na wizara cha matumizi za dawa bila ya kuathiri mazingira ni lita thalathini elfu kwa mwaka na ndio maana tunadhibiti sana madawa hatutaki kuleta madawa kila mtu apate haya yana matatizo ya kuharibu mazingira. Hata hayo maji yaliyokuwa chini ya ardhi yanaweza yakapata sumu yakaja kutuathiri, ingawa hayatatuathiri mara moja lakini pole pole tunaweza kuja kupata athari.

Kuongezeka kwa bajeti ya kifungu cha huduma za utibabu wa mimea wametutaka kufanye hivyo. Nasema fedha zilizokuwa zikitumika kuangamiza maradhi ya mimea zilikuwa zikichangiwa na miradi ambayo hivi sasa imemalizika. Hivyo, fedha zote zimetengwa kutoka serikalini na hali ya serikali tunaijua wakati mwengine tunakuwa na mambo mengi, hivyo fedha zinatengwa zinakuwa kwenye *ceiling* na mambo mengine yanakuwa hayatimii. Kwa hivyo watustahamilie serikali ikipata fedha nyingi basi wizara yangu tutafanya mambo yale tunayoyasema kwa wingi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, walituadhi pia kuongeza fedha kifungu cha umwagiliaji maji. Ushauri umepokelewa pia walituidhi kwamba uendelezaji wa kilimo cha shadidi ushajihishwe. Ushauri huu pia tunaupokea tunaupokea sana kwa sababu shadidi imetoa mwanga kwamba tunaweza tukajitosheleza kwa chakula kama tutafanya hizi taratibu za shadidi. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, wenzetu wakatushauri pia kununua matrekta ya kutosha ili kuweza kutoa huduma zaidi na mapema. Nimesema mwanzo matrekta, kwa hivyo hilo nadhani limeeleweka na naomba Waheshimiwa wawe na imani kwamba serikali itayanunua matrekta hayo. Upatikanaji wa fedha za kutosha za kuendeleza wakala. Mhe. Mwenyekiti, hiyo pia nimeshaisema kwa hiyo tunakwenda haraka haraka. Kwa upande wa Kamati yetu hii ya Kilimo, Biashara na Fedha mambo mengi ni ya kutuaidhi na nasema tumeyakubali yote tutayatekeleza.

Sasa nikienda kwa Waheshimiwa wachangiaji kuna Mhe. Omar Seif Abeid huyu wa Konde yeye anasema kilimo cha mikarafuu kiendelezwe. Kwa ufupi maana yake ni hiyo kwamba kiendelezwe na akashauri tuweke malengo ya mavuno ya karafuu. Tunapokea pia ushauri wako Mheshimiwa na hiyo ndio inayotakiwa kwamba lazima uweke kiwango kwa mwaka huu tutazalisha kiasi hichi na utakachokipata unalinganisha sasa kwa nini tukapata hichi. Kwa hivyo tunapata kujirekebisha. Mheshimiwa ahsante sana kwa ushauri wako tunaupokea.

Jengine akasema miche inagaiwa mingi lakini uendelezaji wa miche hiyo haupo. Tunakubali miche mingi ilipandwa kwa maelfu na maelfu ya miche inatolewa inachukuliwa lakini ukienda huko mashambani utaikuta michache. Hili tunalichukua Mheshimiwa pia na tutalifanyia kazi na nakumbuka tulikuwa Gando tukakutana na kikundi fulani cha mazingira kule tukawaomba watusaidie kufuatilia wakishirikiana na hilimo wafiatilie mambo haya ya miche inayopandwa ili isife.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Omar Seif Abeid akazungumzia habari ya mpunga, wakulima walipata marekta kwa kucheleweshwa. Tutajitahidi tusichelewe kama nilivyokwambia kwamba tukipata matrekta ya kutosha hakuna kitakachochelewa. Lakini pia hali za hewa hizi zikibalika basi inawezekana ukulima usifanyike, wakati mwengine kunakuwa kugumu trekta haliwezi kwenda, wakati mwengine kunakuwa na matope trekta haliwezi kufanyakazi. Kwa hivyo haya yote tuyaone ili tunapokuja kuuliza tuwe tunajua kwamba kuna sababu zilizopelekea kufanya hivyo. Lakini kwa vyovyote vile tujitahidi matrekta yaweze kulima kwa wakati.

Nikienda kwa Mhe. Shaib Said Ali yeye anasema bonde la Mlemele halijaendelezwa. Limepewa ahadi kwamba liendelezwe lakini hakuna kilichoendelezwa. Namshukuru sana kwa moyo wake wa kutaka bonde lile liendelezwe na sisi tutalifuatilia bonde hili ili liendelezwe. Lakini nia ya serikali ni kuendeleza kilimo hichi cha umwagiliaji maji hilo ndio lengo, hakuna bonde litakaloachwa bila ya kumwagilia maji kwa sababu tunataka tuzalishe kwa kumwagilia maji ili haya mazao yaweze kupatikana kwa wingi. Kwa hivyo namuahidi hajasahauliwa mtu bado serikali ina nia ya kuendeleza mabonde yote. Pia akagusia matrekta kama nilivyoeleza kwenye matrekta tena naacha. Akazungumzia jua ya *climate change* mabadiliko ya tabia ya nchi akasema ufanyike utafiti wa kutosha kwani bado kilimo cha kubahatisha. Yeye aligusia hivyo kwamba kilimo tunabahatisha sana wakati tunasema tunapanda kumbe ni kweli wakati mwengine tunachelewa, wakati mwengine tunapanda mapema sana, utakavyofanya kama umekosea miongo ile utakuwa unasababisha mazao kupungua au kutokupatikana kabisa. Kwa hiyo, hili tunalipokea tutafanya utafiti juu ya haya mabadiliko ya tabia ya nchi pia tutazuia sana watu wasiharibu mazingira ili haya mabadiliko ya tabia ya nchi yasitutokee mara kwa mara.

Mhe. Panya Ali Abdalla alisema kwamba kilimo ni uti wa mgongo, nisema mwanzo ni kweli na nakuunga mkono kwa kauli yako hii. Kwa hivyo akatutaka tuhamasishe uzalishaji wa mazao kwa wingi. Sawa ahsante sana Mheshimiwa hilo ndio lengo letu na tutalifanyia kazi kweli kweli. Akasema kwamba bado dhamira tunayo lakini hatujaweza kuifikia. Ni kweli lakini inshaallah tutaweza kuifikia usiwe na wasi wasi Mheshimiwa tuko pamoja.

Pia alitaka kujua maghala mangapi. Kwa kweli serikali ina mpango kabambe wa kuwa na maghala kwa sababu tunajua kwamba inaweza kutokeza dharura kukawa hakua chakula tukawa na ghala zetu kwa miezi miwili, mitatu, sita huko ikaweza kutusaidia. Hapa Unguja ghala moja limeshajengwa na mengine yatajengwa Mhe. Panya Ali Abdalla na ukitaka tukakague tutakupeleka ukakague pia ukatuaidhi zaidi ili tuendeleze ujenzi huo wa ghala kwa namna ile utaona itasaidia zaidi.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, aligusia kuhusu miche lakini tushasema hii kuhusu miche. Pia kagusia kuhusu matrekta tumeshasema. Sasa kwa ufupi nasema mimi nazidi kuwapongeza sana Waheshimiwa

Wawakilishi kwa kukiona kilimo kwamba kinaweza kikatukomboa sana. Kweli kabisa kinaweza kutukomboa na sote tunaamini hivyo. Kwa hivyo tushirikiane mnapoona tatizo basi tuambieni na sisi tuko tayari kuwasikia. Sisi huku tumejinga kufanyakazi kweli kweli lakini na nyinyi kila mkitueleza mnatupa msukumo na tutazidi kuendeleza mambo haya na utafiti ni jambo ambalo kwa kweli tunalitilia mkazo sana kwa sababu hakuna kitakachofanikiwa bila ya utafiti na matumizi haya ya ma-*chemical,* narudia kusema kwamba tutajitahidi sana tutumie madawa lakini kwa viwango ili tusiharibu na mazingira na hiyo mbole kila tutakapopata basi tutaongeza lakini pia hatutasahau kwamba matumizi ya mbolea hasa za *chemical* pia yanaweza kuchangia katika kuharibu mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani nimejaribu kusema haraka haraka kwa sababu muda wa leo ni mfupi naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kabla sijamruhusu Mhe. Waziri kuja kujibu baadhi ya hoja naomba kuna tangazo moja wapo hapa tulisikie kwa ujumla.

Waheshimiwa Wajumbe kwa mujibu wa ratiba yetu baada ya kupitisha Bajeti ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, bajeti inayofuata ni Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Usafirishaji ambayo ilitarajiwa kusomwa siku ya Jumatatu ijayo.

Hata hivyo, kutokana na dharura iliyojitokeza tumefanya marekebisho katika ratiba yetu. Hivyo siku ya Jumatatu ya tarehe 4/06/2018 itasomwa bajeti ya Wizara ya Afya badala ya Wizara ya Ujenzi kama ilivyokuwa awali. Vitabu vya Hotuba ya Wizara ya Afya tayari mmeshapewa kwa hivyo, mvisome mjiandae kwa hilo ili tuweze kuchangia ipasavyo. Ahsanteni.

Sasa naomba nimwite Mhe. Waziri ili na yeye aweze kuja kujibu baadhi ya hoja ambazo hazijatolewa maelezo Mhe. Waziri karibu sana. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:*"Bismilah Rahman Rahim"*. Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote kabisa kwamba naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu Subhana Wataala kwa kutuwezesha kuingia katika siku hii ya leo, siku kuu kwa Waislam, siku yenye neema na tukiwa na afya nzuri katika kukabili mazingira yetu ndani ya mfungo mtukufu wa mwezi huu wa Ramadhani.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nasimama mbele yako mbele ya Wajumbe wa Baraza lako tukufu ili kuweza kufanya majumuisho, majibu ya bajeti yangu ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ambayo pamoja na muda mchache tuliopewa umenipa faraja sana kuona kwamba wachangiaji wa Baraza lako Tukufu wana hamu kubwa sana ya kuchangia wizara hii ambayo ni uti wa mgongo kwa uchumi wa nchi yetu. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, bila ya kupoteza muda nianze moja kwa moja kuchukua nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kuchangia Hotuba ya Makadirio ya Mapato ya Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa mwaka huu wa fedha 2018/19 kwa kina kabisa na kwa hamasa na kwa hisia kubwa kabisa katika

kuendeleza kilimo chetu mifugo, uvuvi na ulindaji wa maliasili ambazo ndio sehemu kuu ya uchumi wetu.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, pia napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wajumbe waliochangia kwa kuzungumza na kuwapongeza sana wale waliofanya jitihada kwa kuleta michango yao kwa maandishi. Hotuba ya wizara hii kwa kweli imepata michango mingi nawashukuru sana Wajumbe pamoja na muda mdogo uliokuwepo.(*Makofi*)

Lakini pia nataka niwahakikishie Wajumbe kuwa michango yao maelezo na ushauri waliotupa kwa kiasi chote tumeipokea, tumeikubali, tutaizingatia na tupo madhubuti kabisa kuifanyia kazi kadri ya uwezo waliotupa Mwenyezi Mungu, hekma ziliopo na tunapokea na kuhakikisha kwamba kadri ya uwezo, maarifa nyanja tulizokuwa nazo tutayafanyia kazi kwa lengo la kuleta mafanikio ya sekta hii ya Kilimo, Maliasili, Mifugo pamoja na sekta ya uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii sasa kumshukuru mwenyekiti wa kamati na wajumbe wake wote wa kamati ya kudumu wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya baraza lako tukufu la wawakilishi kwa michango yao na maelekezo katika utayarishaji wa bajeti hii naomba niwatambue wajumbe wote kwa michango yao mikubwa ambayo wameitowa ndani ya wizara na ufuatiliaji mkubwa waliofanya wakati wa kutafuta kazi ya kutunga bajeti hio.

Mhe. Mwenyekiti, tunaahidi kwamba Wizara itafanya kazi kwa uwezo wake wote na kadri ya elimu iliyokuwepo na wataalamu waliopo kuwatumia katika kufanya kazi kwa maelekezo na ushari uliyotolewa na wajumbe wao.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba niwataje kwa majina kabla ya kuwataja kwa majina Mhe. Mwenyekiti napenda nikujulishe kwamba katika baraza lako tukufu jumla ya waheshimiwa ambao ni wajumbe waliochangia hotuba yangu ni 35, wajumbe hao ikiwa 16 wamepata bahati ya kuchangia moja kwa moja yaani mubashara na wajumbe 17 wamepata fursa ya kuchangia kwa maandishi. Nawashukuru idadi kubwa sana huu ni moyo ambao umeelekeza kuichangia wizara hii ili kuleta mageuzi ya kweli ya kilimo maageuzi ya uvuvi na mageuzi ya kulinda maliasili zetu.

Sasa Mhe. Mwenyekiti naomba niwataje kwa majina waheshimiwa waliochangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Kilimo Maliasili Mifugo na Uvuvi kwa kuzungumza ni kama wafuatao.

1. Mhe. Hamad Abdalla Issa - Makamo Mwenyekiti
2. Mhe. Ali Suleiman Ali
3. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf
4. Mhe. Hidaya Ali Makame
5. Mhe.Suleima Sarahan Said
6. Mhe. Simai Mohammed Said
7. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame
8. Mhe. Mussa Fumu Mussa
9. Mhe. Mussa Ali Mussa
10. Mhe. Mohammed Said Muhammed

11. Mhe. Massoud Abrahaman Massoud
12. Mhe. Omar Seif Abeid
13. Mhe. Miraji Khamis Kwaza
14. Mhe. Shaibu Said Ali
15. Mhe. Panya Abdalla Ali
16. Mhe. Balozi Amina Salim Ali.

Vile vile Mhe napenda niwataje sasa Waheshimiwa kwa maandishi ambao ni:-

1. Mhe.Shehe Hamad Matar
2. Mhe.Bahati Khamis Kombo
3. Mhe.Panya Ali Abdalla
4. Mhe. Lulu Msham Abdalla
5. Mhe. Zainab Abdalla Salim
6. Mhe. Maryam Thani Juma
7. Mhe. Maudline Cyrus Castico
8. Mhe. Hamza Hassan Juma
9. Mhe. Juma Ali Khatib
10. Mhe. Shaib Said Ali
11. Mhe. Mohammed Said Dimwa
12. Mhe. Khadija Omar Kibano
13. Mhe Ali Khamis Bakar
14. Mhe. Said Omar Said
15. Mhe. Miraji Khamis Kwanza
16. Mhe. Hidaya Ali Makame
17. Mhe. Mussa Ali Mussa
18. Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba niweke majumuisho na majibu na kuchangia baadhi ya hoja ambazo zimetolewa katika hotuba yangu. Kabla ya yote naomba nikiri kama nilivyokiri mwanzo kwa Waheshimiwa waliotoa michango, walitoa maoni waliotoa ushauri wote kwa pamoja mapendekezo yao tunayapokea na tunayahidi kwamba tutayafanyia kazi nguvu zao hatutaziacha zielewe hewani.

Mhe. Mwenyekiti, kwa wale ambao wataka kupata kupata majibu nilikuwa na orodha ya watu waliokuwa wakitaka kupata majibu ambao ni Mhe. Nadir, Mhe. Hidaya, Mhe. Simai, Mhe. Dimwa, Mhe. Miraji, pamoja na Mhe. Shaibu, pamoja na kutaka majibu yao ya kina Mhe. tutajitahidi kadri ya uwezo wetu kujibu kwa sekta ambazo tunaziongoza. Kwa hivyo Mheshimiwa naomba watu wote ambao waliochangia nitawaja kwa mujibu wa maeneo walichangia, na mjumbe ajihisi kwamba pale alipochangia nitamgusa kwa namna ya alivyochangia kisekta, nianze na sekta ya maendeleo ya kilimo.Waheshimiwa waliochangia ni pamoja na Mhe. Suleiman Said Sarahan, Mhe. Tatu Mohammed Ussi, Mhe. Mohemmed Said Dimwa, Mhe. Hidaya Ali Makame, Mhe. Omar Seif Abeid, Mhe. Miraj Khamis kwa ujumla Waheshimiwa wengi wamechangia eneo hili la kilimo.

Mhe. Mwenyekiti, katika hoja kubwa zilizoelezwa katika hii sekta ya kilimo ilikuwa ni mabonde kuvamiwa kwa ujenzi, mabonde kuweza kufanyiwa umwagiliaji lakini vile vile kutoa elimu kwa wakulima juu ya mipango ya utumiaji wa pembejeo na kuchangia gharama zake.
Mhe. napenda kuwajibu Waheshimiwa Wawakilishi kwamba katika suala zima la mabonde mle ambao mtahitajika tufuatilie katika bajeti hii ya mwaka 2018/2019 serikali, wizara itafanya jutihada za wazi kufika katika maeneo hayo na kuhakikisha kwamba inasikiliza maeneo ya wakulima na kuweza kutatua maeneo hayo. Lakini vile vile wizara inaendelea na kazi ya upimaji kwa lengo la kupata hati miliki ili kuweza kudhibiti uvamizi unaotokea.

Naamini wazi kwamba wakulima wote wana uwelea wa kutosha juu ya mpango wa utoaji wa ruzuku na pembejeo dawa na kitu chengine, pamoja na kwamba dawa tunapozitoa tunazitoa kwa viwango na utaalamu lakini wakulima wengi wamekuwa na malalamiko ya kukosa dawa zile hususan dawa ambazo zinaondoa magugu, dawa ambazo zimeondoa magugu zina kina maalum na Mhe. Mwenyekiti, na tunazitoa kwa viwango maalum tunawaomba sana wakulima wasipende kuzivamia kwa sababu zina athari ya hali yakimaisha ya binaadamu vile vile hali ya kuharibu mazingira.

Lakini vile vile wizara inanunua pembejeo kulingana na ukomo wa bajeti wizara inagoza kiwango cha ununuzi wa pembejeo kadri ya bajeti inavyopatikana, katika bajeti ya mwaka huu Mhe. Mwenyekiti, naomba nikuahidi kwamba mipango sio mibaya kama tulivyofanikisha vizuri mwaka huu uliopita wa bajeti basi bajeti ya mwakani nayo ina vipaumbele kwani imeongezwa kutoka tani 700 hadi tani 1800 pembejeo hizi zitakapopatikana wakulima wetu hususan wale wakulima wenye vijembe kongoroka na wakulima ambao wanaona mabonde yao hayafanyi kazi vizuri watapata mbegu na pembejeo kwa wakati.

Mheshimiwa katika kupungua kwa fedha kifungu cha SM0101 kilichoelezwa na Mhe. Dimwa programu ndogo ya umwagiliaji maji, kupunguwa kwa bajeti kunatokana na tofauti ya kazi zilizopangwa mwaka 2018/2019 aidha ukulinganisha na 2017/2018 fedha zilizobakia zitatumika kwa mwaka wa pili na watatu wa mradi ambao umepangwa.

Lakini vile vile Mheshimiwa alitaka kujua uendelezaji wa kilimo cha umwagiliaji maji na malalamiko yaliyokuwepo juu ya umwagiliaji maji wizara inaendelea juu kilimo hicho na hivi sasa jumla ya hekta 800 zinatumika kwa kilimo hicho cha umwagiliaji maji, pia heta 520 kupitia *Exim Bank* na hekta 200 kuputia mradi wa *ERPP* zitaendelezwa kama zilivyoelezwa katika kitabu change ukurasa wa 48. Kwa hivyo Waheshimiwa nataka niwatoe wasiwasi, wasiwasi mkubwa ulikuwepo katika mabonde haya kuna mabonde tumeyaweka katika suala zima la umwagiliaji maji, yamekuwa ni maeneo ya uvamizi mabonde haya ikiwa yatafanyika suala la kilimo basi kweli chakula Zanzibar kinawe kikatutosheleza, na wizara itafanya jitihada ya kuyarejesha mabonde hayo katika sehemu ya kilimo na wale ambao wamehamia tutaweza kuwafanyia shughuli nyengine.

Lakini dhana ya shadidi ni kama ilivyo kwa nirika, shadidi ni mfumo wa uzalishaji wa mpunga unaotumia maji kidogo na mbegu kidogo ila inatia mazao mengi teknologia hio imeongeza uzalishaji wa mpunga kutoka tani 3.5 mapaka tani 6 kwa hekta….

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa wajumbe minong'ono imekuwa mikubwa.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Hekta moja ilivyokuwa ikilazisha na hekta moja inavyotarajiwa sasa hivi kuzalisha.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa naomba tumpe utulivu Mhe. Waziri ili hoja zisikilikane. Mhe endelea.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mheshimiwa lakini kwa upande wa nerika ni aina ya mbegu ya mpunga tu lakini shadidi ni teknologia inayotumika katika kufanya kile kilimo cha umwagiliaji maji. Kwa hivyo, Mheshimiwa hata tunapoyatumia haya maeneo yanakuwa yana maana tafauti.

Kuhusu wakulima wa mazao ya viungo wanavunjika moyo kutokana na masoko ni kweli masoko yapo. Wizara ya Biashara tumeshirikana nao katika kuhakikishwa kwamba tutafanya *branding* tutafanya na *production* ambazo zinaonekana zina ubora. Lakini katika kufanya hilo wizara inawahakikishia wananchi na wakulima kwamba mazao ya viungo yana soko la kutosha nadni na nje ya nchi, zao la vanilla linahitajika kwa soko la nje zaidi ya tani 2 kwa mwaka lakini tuelewe kwamba kuivuna vanika kufika tani 2, pilipili hoho na mazao mengine kufika tani 2 ni kazi moja kubwa sana matayarisho yake ni makubwa lakini wizara itaendelea kutoa elimu kwa wakulima ili tuhakikishe kilimo kinawasaidia kama biashara baada ya kuona kwamba kilimo ni pato la kujisaidia siku hadi siku.

Mhe. Mwenyekiti, kuna suala la pilipili manga zao la vanilla kama alivyolizungumza Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda zao hili linapaswa kurejeshwa wananchi warejee kilimo chao kama ilivyotakiwa. Lakini Mhe. Omar Seif Abeid alitaka kujua sana juu mikarafuu ushauri wake kama alivyojibiwa na Mhe. Naibu waziri umepokelewa miche inayotolewa miche inayotolewa pamoja na Wawakilishi wengine walivyouliza tutaifuatilia, ni kweli tumegundua kwamba miche ambayo inatolewa na miche inayohuika mwisho wa mwaka ni tofauti kubwa sana. Idara yetu ya utafiti itafanya utafiti wa kina hali hii na ufuatiliaji tutafanya kwa nguvu zote na tulitaka tuhakikishe kwamba endepo tutagundua wale wananchi wamepata mikarafuu na wameitumia kinyume na mikarafuu basi serikali haitocha kuchua hatua zinazofaa.

Lakini kilimo cha mpunga kama alivyozungumza na kama nilivyokizungumza bado tunaendeleza kufanyia kazi kilimo cha mpunga, nataka niwaahidi kwamba katika kilimo hichi cha mpunga kwa umwagiliaji na mashamba yote yale ambayo yatakuwa yanahitaji kupitiwa na matrekta basi mwaka ujao kuna matrekta ya kutosha tuna mazima 47 ni wazi kwamba tutaanza kilimo kuanzi mwezi wa Oktoba, Novemba na Disemba wakulima wetu waweze kujitayarisha. Lakini nataka nithibitishe wazi kwamb ndani ya bajeti hii imezingatia sana madereva wa matrekta imezingatia sana utengenezaji wa matrekta ili kilimo chetu kianze mapema.

Mhe. Miraji naye ameuliza kupitia rasimu ya wakulima programu wa utawala kama ipo tayari, Mhe. Miraji usiwe na wasi wasi juu ya sera hii, sera hii iko katika matayarisho na iko katika hatua ya mwisho ya kufanyika kazi na michango yako kama unayo huu ni wakati muafaka

wakuileta ili tuweze kuindeleza hiyo sera na michango yako tunaweza tukaipokea na tukaifanyia kazi.

Lakini tukiendela zaid Mhe. Shaibu alitaka kujua juu ya bonde lake la wakulima na wananchi Mhe. Shaibu nataka nikuahidi kwa mguu nitafanya kazi ya kukufata mpaka ulipo na nitashirikiana na wewe na nitakwenda kwenye wakulima wake wako ili tukatatue tatizo ambalo linakubali. Lakini nataka nikuhakikishie tu kwamba matrekta ni kwa ajili ya maeneo yote ya kilimo na mradi wa Korea unaokuja utakufikia katika kilimo hichi cha umwagiliaji.

Katika dawa za kilimo mashambani hususan shamba za mpunga kweli bei inawezekana zinaonekana tofauti inawezekana kuna watu ambao wanakwenda kinyume na maadili ni wajibu wetu wizara kuhakikisha kwamba tunasimia vyema wa zile dawa bei ni moja tu kama tulivyonunulia na bei ambayo tunauzia, lakini kama kumekuwa kuna huo ukikaji wa kisheria ukiukwaji wa kimaadili nakuhakikisha kwamba wizara yangu kama ulivyotoa pendekezo itafuatilia na kuhakikisha kwamba inafanya kazi. Na usiwe na wasiwasi kwa jimbo lako Pujini matreketa kwa mwaka huu mimi nitakuwa wa mwazo kuhakikisha kwamba terketa limefika katika kufanya kazi. Juu ya usimamizi wa mazingira na usimimizi wa mambo mengine ambayo yanafanyika kwenye kilimo nataka kuhakishia Waheshimiwa kama alivyojibu Mhe. Naibu Waziri kwamba mazingira nayo yana mpango wake na kama yalivyoelezwa na Wizara ya Makamu wa Pili wa Rais hivi sasa pia kuna bajeti ambayo tumeika kwa ajili ya kuweka sawa hayo mazingira.

Mhe. Panya Ali Abdalla naye alisema kwamba tumahasishe sana wakulima elimu wizara yangu itaendelea kufanya jitihada ya kutoa elimu za kina kabisa kwa wakulima wa aina zote, hatutachukua ukilima wa umwagiliaji tu lakini nataka niwathibitishie kwamba elimu kwa wakulima inahitajijika ukulima wetu ni mazoea tunahitaji kubadisha ukulima wetu kutoka ukulima wa mazoea twende ukulima wa biashara, kwa hivyo elimu nayo itatumika kwenye vilimo vya aina vyote.

Lakini zile ekari 26,000 kuzigeuza kuwa ekari za umwagiliaji maji ekari za umwagiliaji maji zimekubalika kwa upande mchangani ilikubalika kuwa na ekari 560 lakini kama tulivyosema maeneo mengi yamevamiwa tupo sasa hivi katika mradi unaokuja wa Korea kuhakikisha ekari nyingi sana zitatumika katika kilimo cha kisasa hususan katika kilimo hichi kinachotumia umwagiliaji maji ili kuweza kuvuna zaidi ya mara mbili au tatu.

Lakini Mhe. Jaku na yeye ameungana na Mhe. Panya aliyetaka kujua wakala matrekta wapewe *vote* nawambia hili ni tatizo ambalo liko katika kibajeti. Kwa hivyo bajeti kama ilivyozingatia tumeipanga kwa pamoja na naishukuru sana kamati yetu ya fedha na kilimo kwa kuweza kuzingatia masiala hayo juu ya utengenezaji wa mawakala wa matrekta

Mheshimiwa niingie katika programu ya maliasili. Katika progamu ya maliasili kulikuwa kuna hoja ya Mhe. Simai Mohammed Said wa jimbo la Tunguu ambae alikuwa na hoja ya kujua kwamba kuhusu wananchi wa Ungujaukuu kuzuiliwa kuokota kuni kazu katika misitu ya hifadhi ya Jozoni, ni kweli Mheshimiwa sehemu ya hifadhi zimekuwa zinaharibiwa sana na wizara hivi

sasa ina mikakati maalumu ya kuhakikisha inarejesha rasilimali misitu katika hifadhi zetu hizi za misitu yote iliyipo katika hifadhi.

Na nikupe mfano nzuri tu juzi katika maeno ya Kiwengwa kuna watu walivamia msitu wa hifadhi na kudiriki kujenga majengo ya kiwemo majengo ya ibada na majengo na majengo mengine, na yote wizara yangu imechukua hatua ya kuondosha, lakini hoja hii pia tumeipokea kwa kina Mhe. Said na tutaifanyia kazi. Mheshimiwa nataka nikuhakikishie kwamba hii inapaswa sasa hivi tutoke mguu kwa mguu sisi kama wakakilishi tuwafikie wakulima ambao wanatumia maliasili za kuni katika kuendeleza maisha yao kwa hivyo nataka nikuahidi kwamba mimi na wewe tutafanya ziara ya pamoja tuelekee katika jimbo lako ili tukasaidiane katika kuwakilisha wananchi na kuwasaidia matatizo waliyoyapata. Lakini Mheshimiwa kwa hili nataka nikuhakikishie wazi kwamba bado katika maeneo ya misitu tunalinda hifadhi katika hiyo ili tuweze kuwawekea watalii zaidi.

Katika shamba la mpira Mheshimiwa mashamba ya mipira yenye umri wa miaka 38 yamefika kikomo cha uzalisha kitaalamu wizara kwa hivi sasa ina mpango wa kuyatumia maeneo hayo kwa ajili ya uzalishaji wa viungo na kilimo cha miwa. Kwa hivyo kuna mashamba tayari tumeyatoa ya mipira ambayo ni mikongwe sana yamekatwa na mashamba yamesafiswa na sasa tumeruhu kiwanda chetu ambacho tunakilinda kiwanda cha sukari ili kuweza kutumia shamba na kuweza kilimo cha miwa kuweza kuongeza uzalishaji zaidi.

Lakini Mhe. Panya Ali Abdalla naye aliuliza juu ya eneo la misitu la Chaani, Masingini juu ya hekta zele 440 Mhe. naomba usiwe na wasiwasi wizara yangu imekuwa ikipanda miti kwa kila mwaka katika shamba la Chaani Masingini kwenye maeneo yaliyovunwa hata hivyo pamoja na kuelza kwamba ukikaa upande wa kwanza upande wa pili mtu unamuona kwa kutokushughulikiwa miti ile ndio kama ulivyosiki juzi tumeanza kuongeza ajira tumeanza kutangaza ajira kidogo ili kuhakikisha kwamba tunapata wataalamu ambao wanasimamia na kufuata vitu hivyo.

Lakini bado vipo vitendo vya hujuma vinavyotekea katika maeneo hayo, vitendo hivyo vinafanya na wanachi katika shamba hilo ikiwemo kukata miti na kung’oa miche iliyopandwa naomba sana wananchi waendelee kuziona rasilimali tulizoachiwa na wazee wetu, tumeachiwa kwa faida yetu sisi na sisi tuweze kukirithisha kizazi chetu kijacho katika hali ya kijani ambayo Zanzibar yetu tunajivunia. Kwa hivyo wizara yangu kupitia Idara yangu ya Misitu itaendelea kushirikiana na wewe Mhe. Mjumbe, naomba taarifa zako uzidi kuzileta kwa nguvu ili na sisi tuweze kuzifanyia kazi. Naamini lile lengo ulitaka ujibiwe hapa litakuwa limekaa sawa.

Vile vile Mhe. Mjumbe ulinitaka nikipata muda niende nikatembee kule. Basi nakuhakikishia kwamba bado nipo madhubuti, niko ngangari muda mchache pengine ndani ya huu mwezi wa Ramadhani nitatembea huko pengine na futari inaweza ikapatikana.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, kuhusu watendaji wa shamba la Chaani pia ni wachache sana. Tunakubaliana na hilo, lakini kama nilivyokujibu wizara inakiri na kweli wafanyakazi wa shamba la Chaani Masingini ni wachache na kwa sasa tuna wafanyakazi 15 tu, ni wachache sana kwa ajili ya shamba lile. Lakini wizara inakuahidi itaongeza wafanyakazi kadri fursa za ajira

zitakavyoweza kuruhusu katika Tume ya Utumishi. Sisemi kwamba Wawakilishi ndio watapata nafasi hizi, lakini kwa yule mwenye uwezo na anaye-*deserve* anaweza kupata hiyo nafasi.

Mhe. Ahmada Yahya na yeye alitaja kero za ndege, kunguru ambao wanaharibu, miradi ya kuangamiza kunguru uliokuwa ukitekelezwa na wizara yangu kwa sasa umemalizika, lakini tumo katika mpango wa kuandika mradi mwengine ili tuendelee kuwa na miradi ya kuangamiza wanyama waharibifu katika mazao ya wakulima. Aidha, sumu ya kuulia kunguru inaendelea kutolewa bila malipo kupitia idadi ya misitu. Lakini kama unavyojua akili za kunguru ni kubwa na wana maarifa makubwa sana ya kuzaa. Kwa hivyo ni kitu cha kupambana na bado tunaandikia mradi ili kuweza kuhakisha kwamba tunapunguza idadi kubwa ya kunguru waliokuwepo.

Mhe. Mohamed Said Mohamed Dimwa, ulitaka kujua idadi ya hekta zilizopandwa mikoko inafanana kila mwaka hakuna kinachoongezeka. Suala lako ni zuri sana Mhe. Mjumbe, zoezi la upandaji wa mikoko nataka nikujulishe kwamba ni endelevu, simuoni sijui kama yupo Mhe. Mjumbe, lakini nataka aelewe kwamba kutokana na uharibifu unaofanyika kila mwaka, sekta ya misitu imejiwekea malengo ya upandaji wa hekta 40 za mikoko kila mwaka kwa kipindi cha miaka mitano na endapo hili litafikiwa lengo basi tuhakikishe kwamba mazingira yatakuwa yamehifadhika vizuri. Mhe. Mwenyekiti, tumejaribu kutembelea sehemu za Charawe kutizama jinsi inavyoharibiwa misitu yetu na wizara yetu sasa imepanga mikakati maalum katika kwenda kuendeleza suala hilo, kama alivyouliza Mhe. Miraji Khamis Kwaza juu ya uhifadhi huu wa misitu.(*Makofi*)

Mhe. Suleiman Sarahan Said alitaka kujua juu ya michango ya mikarafuu ambapo suala hili limeulizwa na wajumbe wengi, kuhusu kuchanganywa na vipando vyengine kama inafaa. Je, imeruhusiwa na hakuna athari yoyote ili kupoteza ile mikarafuu yetu ambayo inategemewa. Mhe. Mwenyekiti, kwanza kama alivyojibu waziri Mhe. Amina Salum Ali katika majibu aliyoyatoa hapa. Nataka nimuhakikishie kwamba upandaji wa mikarafuu uliofanyika mwaka 2011 mpaka kufikia mwaka 2016 umekuwa ni mkubwa sana, kama alivyotoa agizo Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuwa ana miche milioni moja kila mwaka na kuhakikisha tunapanda angalau mikarafu mia sita kwa mwaka. Jitihada hii imefanyika kwa nguvu sana, nashukuru sana jitihada za Mhe. Rais na ndio matokeo makubwa ya zao la karafuu la mwaka huu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nataka niwathibitishie Waheshimiwa Wajumbe wote kwamba uvunaji wa karafuu mwaka huu kufikia tani 8,000 umechangiwa kwa kiasi kikubwa na mikarafuu mipya na sio mikarafuu ile ya zamani ambayo tunairithi. Naomba nitowe wito chini ya Wizara yangu ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kuona kwamba tunaendelea na hamasa ya kupanda mikarafuu mipya, mikarafuu inazaa ndani ya miaka mitano hadi miaka sita. Lakini inapofika miaka hiyo mitano inapochanganya mikarafuu uzaaji unakuwa ni mkubwa kuliko uzaaji wa mikarafuu ile ambayo hivi sasa imechoka. Kwa hivyo kwa sasa hivi tutakuwa na mbadala wa kuhakikisha kwamba sera ya upandaji wa mikarafuu inaongezeka.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala lako kwamba kupanda miti mengine mikarafuu ina tabia zake za aina yake peke yake. Mikarafuu kuchanganya na vipando vyengine inafaa wala haina wasi wasi.

Kama mlivyoeleza kwamba Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ina wataalamu na mnawaona juu kweli wataalamu wapo na wamethibitisha hili kwa kutumia tafiti kwamba inafaa kuchanganyisha. Katika miaka mitatu ya awali miaka hiyo ambayo inakuwa vinapandwa vile vipando vyengine hakuna athari yoyote ambayo inajitokeza. Lakini miaka inayofuata uchanganyaji wa mikarafuu na miti mengine unatakiwa uwe wa hadhari kubwa ili kuepuka kukauka kwa mikarafuu kutokana na ukataji wa mizizi. Kwa hivyo tuwe makini sana tunapokata mizizi ya miti yetu mengine tunayotoa ili tusije kuiathiri ile miti ya mikarafuu ambayo itasababisha kuondoa uhai wa kuishi kwake.

Mhe. Nadir Abdul-latif ulitaka kujua wizi wa mchanga Chaani Ketwa uliofanywa na ndugu Babla pamoja na wizi wa kifusi. Hatua tayari zimechukuliwa na kuhakikishia kwamba tutasimama kwa hatua zote na taarifa tutakupatia Mhe. Nadir Abdul-latif juu ya hatua ambazo tutazichukua. Suala hili tayari limefika ndani ya wizara yetu, imezifuatilia vibali vya uchukuaji wa mchanga mali zisizorejesheka, gari tano zilihusika na wizi huo na wizara pia ilipeleka taarifa hizo katika vyombo vya sheria kwa hatua ya kisheria katika suala hili na sisi tutafuatilia mpaka tuhakikishe kwamba haki ya yule mama nayo imetendeka. Serikali yetu haina dhamira ya kumuonea mtu yeyote katika kupata haki yake. Kwa hivyo tunakuhakikishia kwamba tutafuatilia ili haki ifanyike na mama mwenye bonde lake tuone namna gani amepata haki yake.

Vile vile Mhe. Machano alisema kuwa alirejeshee eneo hilo alilolichimba mchanga. Hatua hizo hivi sasa tumo katika kuzitafiti kitaalamu ili tujuwe ni namna gani maeneo yaliyoathirika. Suala hili pia limeelezwa sana na Mhe. Miraji Khamis Mussa, alitaka kujua mpango wa serikali ambao umepanga namna ya kuyarejesha maeneo yaliyochimbwa kifusi, mawe na mchanga. Ni kweli mazingira ndani ya visiwa vyetu tumeyaharibu kwa matumizi ambayo yametusaidia kwa manufaa yetu sisi wenyewe. Lakini nataka nikuhakikishie Mhe. Mjumbe kwamba tayari tumekuwa na mpango wa kurejesha upandaji wa miti ambao utarejesha uoto wa ardhi katika sehemu hiyo. Kabla ya kurejesha tumekuwa na mipango ya kuhakikisha kwamba tunaweka *filling* ya kwanza ndio tunaipa nafasi ya miti kuipanda katika sehemu hizo.

Mhe. Mwenyekiti, niingie katika programu yangu ya tatu ya mifugo ambayo haikuwa imeulizwa kwa kiasi kikubwa. Hoja iliulizwa na Mhe. Suleiman Sarahan Said wa Jimbo la Chake Chake juu ya uchinjaji wa mifugo katika maeneo yasiyo rasmi. Uchinjaji wa mifugo kisheria umewekwa katika maeneo maalum yaliyotengwa ya uchinjaji unaofanyika nje ya maeneo hayo ni kinyume cha sheria. Kwa hivyo vyombo vinavyohusika vinapaswa kuchukua hatua zinazostahiki.

Mhe. Omar Seif Abeid na yeye kuhusu kufuatilia wizi wa mifugo. Tunasema kwamba ushauri wako tunauchukua nanahakikisha kwamba tutasimamia kama alivyouliza Mhe. Nadir Abdul-latif na wajumbe wengine. Kuhusu wizi wa mifugo kweli una kera, una udhi na ni janga kwa taifa letu. Kwa hivyo kwa kushirikiana na Wizara yetu ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mkoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kama tulivyosema tuna vijana na wanaweza kufanyakazi. Sisi tayari tumeanza kuingia katika mikataba, tumeingia mikataba na Vikosi vyetu vya Kazi Maalum ili tuwe tuna walinzi ambao wanaweza kuifanya hii kazi ya kukamata hawa wezi. Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nithibitishe kwamba bila ya kuoneana haya tutakapowakamata wizi, wawe watoto wetu, watoto wa waheshimiwa au watoto wengine, tutakapowakamata na hatua zitakapochukuliwa wizi ndani ya visiwa hivi utaondoka.(*Makafi*)

Mhe. Shaib Said Ali na yeye aliuliza juu ya suala hilo juu ya wafugaji tutawasaidiaje ulinzi na kusaidia kupunguza wizi. Nataka niwaambie wafugaji wote pamoja na wakulima kwamba wizara yetu ni yao, wanapaswa kuwa karibu na wizara yetu waje wanapokuwa na matatizo, kushirikiana kwetu na kufanya mikutano ya pamoja ndipo tutakapoweza kutatua tatizo hilo.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niende na hoja ya uvuvi ambapo Wajumbe wamezungumzia kwa kina zaidi. Mhe. Mohamed Said Mohamed Dimwa nashukuru sana juu ya suala lako la uchukuaji wa takwimu za uvuvi. Sio za ukweli. Mhe. Mwenyekiti, nimejaribu kuingia katika *Hansard* asubuhi hii ya leo na nimekwenda kusoma kwa muda wa nusu saa juu ya *Hansard* ambazo zinajibiwa tangu mwaka 2010 ilipoanza awamu hii ya Mhe. Rais wa Zanzibar ambaye ana machungu na suala zima la uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nikuthibitishie kwamba kama uchungu aliokuanao Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, juu ya kuinua suala zima la uvuvi na kuwawezesha wananchi wake kuweza kuingia kuvua bahari ya ndani, bahari ya kati na bahari ya juu. Basi nataka nikuhakikishie kwamba takwimu hizi zinachukuliwa kitaalamu na hivi juzi tu tulialika meli ya kuchukua takwimu za uvuvi wa samaki na mazao ya baharini na takwimu hizo kama tulivyozisema zitakapokuwa tayari tutazileta.

Mhe. Mwenyekiti, lakini uchukuaji wa takwimu za uvuvi ni kweli kama ulivyosema ni za ukweli ambao unafuatana na mfumo maalum unaojulikana kwa jina la "*Catch Assessment Survey* (*CAS*). Mfumo huu hutumiwa na wakuu wa madiko baada ya kupata mafunzo ya kitaalamu ambayo ni upimaji wa samaki kwenye vituo maalum vinavyochaguliwa, hata kwetu kule Uroa kipo kituo hicho na mchukuaji wa takwimu hizo anaitwa Hashim Salum Mchenga na yeye kila siku kinachovuliwa pale anaweza kurekodi na kuwasilisha katika Wizara yake ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi. Kwa hivyo takwimu zinazochukuliwa ni za sahihi.

Mhe. Suleiman Sarahan Said na yeye alikuwa na suala zito juu ya samaki watakaovuliwa bahari kuu watatumiwa kwenye soko la ndani au nje pia. Nataka nikuhakikishie kwamba Mhe. Mohamed Said Mohamed Dimwa alifanya kazi nzuri mwaka 2013, kazi ambayo leo anaipinga mwenyewe, lakini ndio mambo unasahau unakotoka hujui unakokwenda. Nataka nieleze wazi kwamba kazi aliyoifanya Mhe. Mohamed Said Mohamed Dimwa ya kuweza kuhakikisha uvuvi ndani ya bahari kuu na bahari ya kati kutumia vyombo vya kisasa unafanyika, kazi hiyo sasa inaendelea na ndio maana tukaanzisha hili Shirika la Uvuvi la *ZAFICO*.

Mhe. Mwenyekiti, juzi tu tulikuwa na safari tulitembelea nchi za nje na juzi tulikuwa tuna mkutano wa Kamishna, lakini mikutano hii yote imeonesha mafanikio ya hali kubwa ya uvuvi ndani ya bahari yetu ya *Indian Ocean* ambayo itatupa matumaini makubwa ndani ya ajira kwa wananchi wetu hapa wa Zanzibar. Kama tulivyoeleza katika bajeti yetu, tayari tumekuwa tunasomesha vijana wetu ili kuweza kwenda kushirikiana na meli ambazo zinasajili kuja kuvua hapa, basi tayari samaki hawa tutawafanyia *Industrial Processing Pack* hapa hapa Zanzibar, tutafanyia vyumba vya baridi hapa hapa Zanzibar na wanaotaka kununua watanunua kutoka hapa Zanzibar ili waelekee nchi za nje. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mikakati na sheria tunazipanga na kampuni yoyote inayotakiwa kuja kufanyakazi hapa itashirikiana na Kampuni yetu ya Uvuvi ili kuhakikisha kwamba haya yote yanafanikiwa na uvuvi wa Zanzibar unarudi kama ulivyo wakati wa asili. Kwa hivyo Mhe. Mohamed Said Dimwa nashukuru sana katika kuzungumza kifungu cha 19(1) ndicho kilichopelekea kutungwa kwa Kanuni ya maeneo ya hifadhi ya *MSU* ambayo Mhe. Dimwa wakati ule ulikuwa una hamasa kubwa na sisi tunakushukuru kwa kazi yako kubwa uliyoifanya na tunaiendeleza, na tunakuhakikishia kwamba tutaifanya kwa vizuri kama ilivyoonekana dhamira yake kwenye Toleo Nam.6528 ya Sheria ya kuunda hifadhi hiyo. Lakini Kanuni hii imeonekana kuwa na mapungufu kidogo na wizara iko katika utaratibu wa hivi sasa wa kuzirekebisha Kanuni hizo ili tuhakikshe kwamba raslimali zetu...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, malizia muda wako ili tuweze kupata muda.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Namalizia. Raslimali zetu ambazo zinachukuliwa kwa wingi nazo tunazirejesha.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, nataka kukujulisha kwamba zabuni ya ujenzi wa soko la Malindi, la yule mjumbe aliyeuliza kuhusu soko la Malindi litajengwa lini, Mhe. Jaku Hashim Ayoub aliuliza suala hilo. Nataka kuwathibitishia kwamba *tender* tayari zimepitishwa na kampuni tayari zinafanyakazi yake ya uratibu na soko wakati wowote linaweza likachelewa kidogo ndani ya miezi minne kutokana na utaratibu wa kampuni ya Japan, lakini taratibu hizo zinaendelea.

Vile vile nataka kuzungumzia kwamba wizara kwa kupitia utaratibu wa maeneo ya hifadhi kuwasaidia wavuvi vifaa. Inawasaidia wavuvi vifaa na sio fruweli za baiskeli Mhe. Mwenyekiti. Vifaa vya uvuvi, mimi mwenyewe ni mmoja katika hithibati kwa sababu kijiji chetu ni kijiji cha uvuvi. Lakini nataka niwahakikishie kwamba wizara itaendelea kuwasaidia wavuvi, kama tulivyofanya mikutano mbali mbali katika kuyafanyia hivyo kwa kupitia kamati zao za uvuvi.

Mhe. Hidaya Ali Makame na yeye aliuliza vihori vinavyokusudiwa ni kwa ajili ya wakulima wa mwani. Vihori vile vinavyotolewa kimoja kimoja ni kwa ajili ya wakulima wa mwani. Wavuvi tutawasaidia kwa zana za uvuvi na mwani tumesema unatakiwa upandwe katika kina cha maji kirefu. Kwa hivyo tutawasaidia vihori na zana nyenginezo ikiwemo tari, vile vijiti vya kupandia na vitu vyengine ili waweze kufanya kazi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie katika mipango ya utawala kabisa. Mhe. Mohamed Said Mohamed Dimwa ninapenda kumjibu kwamba kwa kipindi cha miaka mitatu, nafasi 312 za ajira kwa ajili ya mabwana shamba na mabibi shamba na wale walioiuliza kuhusu mabwana shamba na mabibi shamba pamoja na ugatuzi tutakaoufanya mwaka huu, lakini mabwana shamba na mabibi shamba ndio kazi yao kufika mashambani. Endapo walikuwa wanadorora na hawatekelezi kazi zao basi wizara yangu itaendelea kufanya jitihada za kuwasimamia. Hata hivyo maafisa hao kwa sasa wamo katika mpango wa ugatuzi na hivyo zoezi hili litaendelea na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Lakini wizara yangu pia ina wafanyakazi wa kada ya ulinzi katika visima na *pumps*. Hilo nalo napenda kulielezea kabisa ili lijulikane.

Mhe. Mwenyekiti, namalizia juu ya suala la chazo ambalo limeulizwa na Mhe. Shehe Hamad Mattar, wewe mwenyewe Mhe. Mwenyekiti kama ulivyo. Mhe. Miraji Khamis ananiuliza. Lakini muda basi unaweza ukaja nafikiri nitamjibu majibu yake tunapoendelea pale.

Mhe. Mwenyekiti, wizara inakusanya takwimu za mazao ya kilimo kwa kupitia mabwana shamba na mabibi shamba na takwimu zimethibitishwa na Mtakwimu Mkuu wa Serikali. Namshukuru sana Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi. Lakini nataka kumuhakikishia kama alivyotoa majibu yake kwamba Mhe. Miraji Khamis Mussa mashimo yaliyochimbwa mchanga tutayarejeshea, tutatangaza *tender* kwa wenye uwezo, ikiwa wazalendo watakuwepo wenye kuyarejesha mashimo na uharibifu wa mazingira, basi tupo katika mpango maalum serikali ya kuhakikisha kwamba mashimo yale tunayarejesha.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache najua kwamba kuna masuala mengi yalitakiwa kujibiwa, lakini muda kila nikitizama nao unaonekana ni mfupi. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba michango yao tunaithamini kwa kiasi kikubwa sana, michango yao inajenga wizara yetu na ina lengo la kuendeleza wizara yetu na tunawahakikishia kwamba tutaifanyia kazi. Ninapenda kuwaambia Waheshimiwa Wajumbe wizara yetu ni wizara yao, tuwe karibu na wizara, walete yale ambayo wanayapata, waache yale tu watakayochukua kwa wafanyakazi, lakini wanayoyapata kwa lengo la kuijenga wizara yetu basi watuwasilishie ili tuyafanyie kazi kwa pamoja.

Baada ya hayo machache Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru wewe, nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe waliotoa hoja. Naamini kwa hoja hizi tulizozitoa Wajumbe wengi watakuwa sasa tayari kuipitisha bajeti yangu bila ya tatizo lolote, ili watupe fursa tukafanye kazi tuachane na yaliyopita. Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, kabla hujatoa hoja. Nimepata ujumbe kwa kuweka *Hansard* sawa kuna Waheshimiwa Wajumbe, wamechangia hujawataja. Mhe. Makame Said Juma na Mhe. Tatu Mohamed Ussi. Naomba uwatambuwe na hao.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwaingiza katika *Hansard* Mhe. Makame Said Juma na Mhe. Tatu Mohamed Ussi. Nilisema Mhe. Tatu Mohamed Ussi kwamba alichangia na ndipo nilipotaja lile suala la kule upande wa Mkoa wa Kaskazini. Sitaki kutaja tena kwa jina. Lakini nawashukuru sana kwa michango yao na naomba majina yao yaingie katika *Hansard* kwamba ni watu ambao wameisaidia bajeti hii kuichangia na kupelekea maendeleo na mageuzi ya kilimo kwa wakulima, wakwezi na wavuvi. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nashukuru. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

MICHANGO YA MAANDISHI

WIZARA YA KILIMO, MALIASILI, MIFUGO NA UVUVI

Mhe. Said Omar Said: Mhe. Waziri kwanza napenda kukupongeza kwa umahiri wako wa kuongoza wizara kwa umakini na ufanisi.
- Nataka nianze mchango wangu kwa ombi la dharura lifuatalo;

Nimepata taarifa kwamba, katika mabonde ya Koowe na Ukele katika Jimbo la Wingwi kumetokea maradhi ya mpunga ndani ya wiki hii tuliyotokana nayo.

Hivyo, naomba hili ulitafutie ufumbuzi wa dharura na unieleze bayana hatua gani utakazochukua ili yanusurike na maeneo mengine, ambayo hayajaathirika katika mabonde hayo. Naomba unipe ufafanuzi utakapokuja kwenye majumuisho.

- Mchango wa pili ni kuhusu mabwana shamba. Kwa kuwa tunao mabwana shamba wetu wajitahidi kufanya ukaguzi katika maeneo yao ya kilimo mara kwa mara, ili kama kuna tatizo aweze kulifanyia marekebisho kabla ya kutokea athari. Wakulima wanalalamika sana kukosa kuwaona mabwana shamba.

- Mchango wangu wa tatu ni kukosekana dawa za kuulia magugu kwa wakulima, wakulima wanasumbuka sana, tunaomba tupatiwe huduma hii ili wananchi wajengeke imani ya kurahisishiwa kazi.

- Mchango wangu wa nne ni kuhusu wataalamu wa kilimo. Mhe. Waziri wakulima wetu wanajitahidi kufanyakazi ya kilimo kwa juhudi kubwa, lakini juhudi zao mara nyingi hazileti na zaidi hupata hasara kwa kugharamia kilimo hicho kwa fedha nyingi. Hebu tujiulize ni kwa sababu zipi.

  Wakulima wetu wanahitaji hata maelekezo ya jinsi ya kutumia mbolea. Kwa hivyo, mimi nadhani kwamba kukosa maelekezo ya kilimo kutoka kwa wataalamu wetu kutakuwa hakuna tija kwao.

  Baada ya mchango huu naunga mkono hoja. Lakini naomba unijibu niliyotaka ufafanuzi. Ahsante.

Mhe. Mussa Ali Mussa: Mhe. Waziri naomba Wizara yako ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kutupatia matrekta kwa wakati pamoja na pembejeo na mabwana shamba.

Mhe. Waziri, naomba uongeze fedha kwa ununuzi wa madawa ya kuulia magugu, madawa ni muhimu sana.

Mhe. Waziri, naomba katika bajeti yako ya mwaka huu ununue ng'ombe wa maziwa wapatiwe wafugaji kwa mpango aw kopa ng'ombe ulipe ng'ombe. Ahsante.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Mheshimiwa, mimi nataka kuchangia kuhusu suala la ajira katika wizara yako bado ni changamoto hususan kwa vijana wetu waliomaliza masomo yao katika Chuo cha Kilimo Kizimbani.

Je, ni utaratibu gani ambao utatumika au utauchukua ndani ya bajeti hii ambayo tunatarajia kuipitisha muda mfupi tu kuanzia sasa hivi?

Tunahitaji kauli yako yenye kutia moyo wananchi wetu hususan vijana wetu wa Zanzibar. Pia suala la malipo fidia kwa wale watu waliokodishwa mashamba yao na kuambiwa kwamba

watalipwa fidia nampaka muda huu yamefikia hatua gani? Utaratibu gani utaendelea kutumiwa kwa ulipwaji wa fidia zao wakulima hao.

Pia ningeomba maelezo kiukamilifu juu ya ukarabati wa majengo ya wizara ya kilimo, hususan majengo yaliyoko maeneo ya Chuo cha Kilimo Kizimbani, yaani ofisi za kilimo na kuhifadhi matrekta. Majengo yale yameshakua ya miaka mingi sana mpaka kufikia kuonekana majengo yale hayana washughulikiaji.
Nahitaji maelezo juu ya suala hili na nina nia ya kuzuia kifungu juu ya suala hili la uchakavu na ubovu wa majengo hayo ya ofisi. Naunga mkono hoja baada ya kupata ufafanuzi. Ahsante.

Mhe. Khadija Omar Kibano: Mheshimiwa, nawapongeza wakulima hao waliyojitokeza kwa mashirikiano yao ya majimbo mawili haya ya Gando na Mtambwe, kwa kushajihishana kwa pamoja ili kuunda *SACOS* ya wilaya ya kilimo cha Vanila.

Ombi langu kwa wizara iendelee kuwashajihisha wananchi mbali mbali wa Unguja na Pemba kwa kilimo cha Vanila ili waukuze mradi huo.

Changamoto iliyojitokeza ni uhaba wa miche, wakulima wapo lakini miche hapana. Mhe. Waziri kuwe na nasari ya wizara ili waweke miche ya Vanila na mikarafuu, ili mkulima anapohitaji miche aipate kirahisi.

Hivi sasa kilo moja ya Vanila ni shilingi 800,000/- kwa soko la ndani, sijui huko duniani.

Ushauri wangu. Mhe. Waziri, naomba mkae pamoja Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi na Shirika la *ZSTC*, kwa mashirikiano ya pamoja, ili Vanila wanunuwe wao kama inavyonunuliwa karafuu na Zanzibar.

Kwa kuepukana na walanguzi tutaongezea pato la nchi yetu. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Mchango wangu ni kwamba Wilaya ya Maweni ni moja ambayo ina wafugaji wengi. Kwa miaka mingi ilikuwa wanyama wao wakichan'jwa kwa kipindi cha miezi 3 mitatu kila mwaka, jambo ambalo sasa hivi limekosekana;

Je, utaratibu huo umeondoshwa? Hatuoni kukosekana kwa huduma hii ndio kutaleta wanyama hao kuwa na maradhi.

Wakulima wa mahindi, mtama, uwele na mpunga, wakulima wa Micheweni, Kiuyu, Maziwang'ombe, Kojani, Makaani na Mjini Wingwi hulima sana mazao hayo na kutokana na mabadiliko ya tabia ya nchi, hukosa hata mbegu za kuatika katika siku za mbele.

Je, wizara ina mpango gani kwa wakulima wale kuwapatia elimu juu ya jambo hili na kuwasaidia kwa pembejeo? Lini wizara itatoa fidia kwa wakulima wa mazao haya yaliyoathirika sana?

Kuhusu suala la mifugo, tumeona kuwa maeneo mengi yamevamiwa kwa kilimo na kukosa wafugaji kupata eneo la malisho ya wanyama wao.

Je, ni lini wizara itatoa maeneo maalum ya malisho ya wanyama na kuondosha kadhia ya wafugaji na wakulima kugombana.

Kuhusu madereva wa matrekta wanafanyakazi zaidi ya masaa yao ya kazi na tumeona kuwa bado hawafikiriwi kwa kutoa fedha za muda wao huo.

Je, ni lini wizara itawafikiria kwa kuwapa pesa za overtime yao.

Vile vile naipongeza Serikali ya China, iliyotoa tender kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa kununua muhogo na kwakua Zanzibar wapo wakulima wengi na itatoa ajira nyingi.

Je, wizara imelifuatilia jambo hili kwa kina kujua uhalisia wake?

Ni lini wizara itatoa tangazo juu ya wananchi ili waweze kulima zao hilo?

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, naongezea mchango wangu kwa kuwa nahitaji ufafanuzi wa baadhi ya mambo na kwa kuwa muda haukunitosha.

Katika ukurasa wa 101, kuanzisha kituo cha karantini ya mifugo huko Gando Pemba. Nilitaka kujua kama hati ya umiliki wa ardhi imepatikana.

Je, wananchi wa pale waliofanyiwa tathmini ya vipando (mazao yao) wameshalipwa mafao yao. Hatua gani kwa sasa inayoendelea?

Kituo cha Fuoni kwa sasa kimezungukwa na nyumba (mtaani) kwa sasa na josho la pale tayari limejengwa nyumba za makaazi na halifai tena. Wizara imechukua hatua gani au ile ardhi ya pale imeuzwa.

Ukurasa wa 102. Nziwengi imetengewa kiasi gani kujenga uzio na kiasi gani kimetengwa kwa vipando.

Kuongezeka kwa kunguru. Wizara ina mpango gani kwa sasa wa kupunguza kunguru, kwa sababu wamekuwa wengi sana na ulikuwepo mradi wa taaluma ambao watendaji wetu. Hivyo, wizara imejipanga vipi au wale waliopewa taaluma hawapo tena. Ahsante.

Mhe. Shaib Said Ali: Mchango wangu wa maandishi kwa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya shukrani kwako, waziri na kwa watendaji wake wote wa wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri anielezee ni lini bonde la Mlemele Pujini litaanza kutekelezwa kwa kilimo cha umwagiliaji, kama bajeti ya tatu sasa inavyoahidi. Naunga mkono hoja. Ahsante.

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchangia kwa maandishi. Mhe. Waziri nikupongeze wewe na watendaji wako wote.

Mhe. Waziri, naomba ukiangalie sana Kiwanda cha Kusarifu Mazao Pujini, ili tupate wafanyakazi wazuri na waweze kuwahudumia wananchi, hakuna wafanyakazi wazuri.

Majembe ya kulimia yafike mapema kuwalimia wananchi. Pia wananchi walazimishwe kulima kilimo cha shadidi kwa manufaa yao wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

Mhe. Zaina Abdalla Salum: Mhe. Mwenyekiti, na mimi naomba kuwasilisha mchango wangu wa maandishi katika hotuba ya Waziri wa Kilimo, Malisili, Mifugo na Uvuvi, kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa hotuba yake nzuri iliyojaa mafanikio ya uchumi wa nchi yetu na wananchi kwa ujumla. Pia kuna changamoto mbali mbali, ambazo changamoto hizi hufanya utekelezaji kuonekana kuwa ni hafifu, jambo kuwa hatua za utekelezaji huwa zinachukuliwa, lakini bado zinaendelea kujitokeza hatua kwa hatua.

Mhe. Mwenyekiti, kilimo ndio uti wa mgogo wa nchi yetu, kwani wananchi wengi wa Zanzibar wanategemea sana kilimo kwa mazao mbali mbali, kwa chakula na biashara. Kwa dhati kubwa kabisa niipongeze Serikali ya Mapinduzi na kwa utawala wa Rais Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kuiboresha sekta hii ya kilimo na katika uingizaji wa matrekta, kwani kwa sasa wakulima wetu wameanza kurahisishiwa katika kulima na kuondokana na kilimo cha zamani, ambacho walikuwa wakitumia mikono na nguvu nyingi.

Mhe. Waziri, matrekta hayo kwa sasa yamekuwa ni biashara kwa wakulima wetu na imekuwa ni mtihani sana, kwa sababu leo mkulima analimiwa shamba nusu heka kwa shilingi 50,000/-.

Bonde la mpunga dawa chupa shilingi 30,000/- na nusu heka chupa mbili na mpigaji wa dawa atatakiwa mkulima amlipe mpigaji dawa shilingi 10,000/- kwa kila chupa. Kwa hivyo, Mhe. Waziri, bado tunatakiwa tuwaangalie sana wakulima wetu na hasa ukizingatia wakulima wengi wao hulima mazao kwa matumizi ya nyumbani. Kama mpunga wengi wao huwa wanalima kwa matumizi yao na familia na sio kwa biashara.

Mhe. Mwenyekiti, zao la mizizi kama vile viazi vidogo vidogo yaani mbatata, limekuwa halitiliwi mkazo kwa wakulima, kwani zao hili ni zao ambalo sana tunategemea kutoka Tanzania Bara, sana hapa kwetu huwa halipatikani kwa kiwango kikubwa. Sasa nikuombe tu Mhe. Waziri liboreshwe zao hili ili lilete tija kwa wakulima wetu na watumiaji, kwani zao hili ni la biashara na linaweza pia kuongeza pato la nchi yetu.

Mwisho Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Mhe. Mwenyekiti, mchango wangu wa maandishi kwa Wizara ya Kilimo, Malisili, Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti, nampongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote, kwa maandalizi ya hotuba hii pamoja na uwasilishaji kwa umakini.

Mhe. Mwenyekiti, mchango wangu unaanza katika ukurasa wa 3 - 8, juu ya ukuaji na mchango wa sekta ya kilimo katika pato la taifa kwa upande wa takwimu zilizopo katika kurasa hizo. Je, chanzo chake ni wapi.

Kwa mfano, takwimu za mazao ya chakula cha ziada kwa ajili ya biashara katika uzalishaji. Kama muhogo, ndizi, viazi vitamu na vyengineo. Vile vile kwa upande wa mazao ya kilimo cha mbogo mboga sijapata kuona mtu anachukua takwimu hizo, ama kuja shambani au akiwa sokoni na masoko ni mengi. Je, takwimu hizi zimechukuliwa hatua gani?

Hata hivyo, wamesema maeneo ya kilimo cha maweni kwa upande wa mboga mboga kumeongezeka. Je, wamepata vipi takwimu hizi, wakati mimi nilikuwa ni mkulima lakini sijawahi kuwaona maafisa au mabwana na mabibi shamba kufanya ziara katika kuwatembelea au kuona angalau dodoso lenye maudhui hayo. Naomba utakapokuja unipe maelezo.

Kuhusu ukusanyaji wa mapato nawapongeza kwa kuvuka lengo, lakini wasisahau kulipa deni la asilimia 40 ya mkulima wa mashamba ya mikarafuu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nishauri Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, ili kulinda viwanda tunavyokusudia kuvianzisha hapa nchini. Ni lazima tujiandae na malighafi za viwanda hivyo ni kilimo cha michikichi.

Faida ya kilimo hichi ni nyingi kama;

a) Kinahifadhi maji ardhini
b) Chakula cha nyuki
c) Upatikanaji wa mafuta aina ya mawese na chikichi ambayo ni mazuri kwa chakula cha binadamu
d) Chakula cha kuku

Mhe. Mwenyekiti, naomba niishauri wizara katika kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi, kuwatafuta na kuwashajihisha wananchi kupanda miti ya misitu na kutunza pamoja na kuwatafuta ambao tayari wanayo misitu yao ya asili na kuwapa elimu ya kutunza na kuendeleza pamoja na kuwapa motisha.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri. Waheshimiwa Wajumbe sasa hoja imetolewa na imeungwa mkono. Naomba niwahoji wale wanaounga mkono hoja ya Mhe. Waziri, wanaokataa. Waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali hotuba ya bajeti ya Wizara yangu ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi. Sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi vya wizara yangu bila ya mikwaruzo. Ahsante Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU A01 - WIZARA YA KILIMO MALI ASILI MIFUGO NA UVUVI

Kifungu A0101 Ofisi Kuu Pemba

Mhe, Mwenyekiti: Mhe. Suleiman humo katika mtu uliyesema utachangia, kwanza ni mapato hayo. sijaona orodha ya watu waliosema kwamba unaweza kutoa hoja hii.

Kifungu A0101	Ofisi Kuu Pemba	996,000,000
Kifungu A0104	Idara ya Misitu na Mali ya Asili zisizorejesheka	8,149,000,000
Kifungu A0108	Idara ya Kilimo	75,000,000
Kifungu A0109	Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Kizimbani	140,000,000
Kifungu A0110	Idara ya Maendeleo ya Mifugo	90,000,000
Kifungu A0111	Idara ya Maendeleo ya Uvuvi	

Mhe. Mohammed Said Dimwa: Mhe. Mwenyekiti, wakati ni kichangia nilionesha kusikitishwa na kushuka kwa mapato ya bahari kuu na Mhe. Waziri alipokuwa akinijibu ipasavyo kwa nini mapato haya yameshuka kiasi kikubwa sana. Nilikuwa naomba ufafanuzi huu kwanza.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza napenda nikiri kwamba kama alivyoeleza Mhe, Dimwa kwamba mapato yanaonekana yameshuka katika suala la uvuvi vya baharini kuu, lakini mapato ya uvuvi wa bahari kuu inatokana na usajili. Chanzo kikubwa cha mapato pale ni utoaji wa leseni na usajili wa zile meli ambazo zinakuja kuvua hapa. Kwa hivyo wingi wa meli zinazokuja kuvua na uchache wa meli zinazo kuja kuvua nazo ndizo zinazosababisha kuwa na mapato juu na kuwa na mapato ya chini.

Hivyo kwa kipindi hichi alichokiona kuwa mapato yameshuka ni pamoja na utaratibu ule wa usajili wa leseni za meli.

Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nimemfahamu sana Mhe. Waziri wakati akilizungumza suala hili lakini kuna Kanuni zimebadilishwa pale ndio wateja wetu *clients* wetu wanaokuja kununua leseni zikapungua na tumefika pahala pesa hizi asilimia hamsini 50 zinakwenda ni *operation cost* lakini asilimia thelathini 30 zinakwenda Bara na asilimia 20 zinakwenda wapi. Hofu yangu hata hizi asilimia 20 kama tutaendelea na Kanuni hizi kuzibadilisha tutakuwa hatuwezi kuchangia kwenye bajeti, nilikuwa nataka kujua. Kwa nini Kanuni hizi zimebadilishwa hata meli zimekimbia, hatuwezi kupata pesa hizi kwenye bajeti.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana ninapenda kumfahamisha Mhe. Dimwa kama nilivyojaribu kueleza kwamba kwanza namshukuru, kuwa yeye kuwa ni mmoja katika walioshiriki kuzitengeneza zile Kanuni tangu mwaka 2013/14 na hii, lakini nataka nimueleze wazi kwamba hivi sasa tupo katika mchakato wa kuzibadilisha Kanuni hizi, hilo ni suala la kwanza na wakati wowote Kanuni hizi mapungufu tuliyoyaona, kama vile alivyoyaona yeye yatakuwa yameondoka katika muda mfupi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini vile vile nataka nimueleze kwamba hiki ni Kitengo kinachoshughulikiwa chini ya serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ndio maana kinaleta ule mgao na mgao huo tumeukubali na madaraka tumekubaliana nayo hivyo, tunabadilishana kwa zamu, ifikapo Disemba itakuwa ni zamu ya Zanzibar kushika ule ukuu wa ile Idara, wale watakuwa wamemaliza. Kwa hivyo pia itakuwa ni nafasi nzuri kwa Zanzibar kuona kwamba ile asilimia ishirini 20 nayo inatumikaje. Nataka nimuhakikishie tu Mhe. Dimwa kipindi cha nyuma mapato ya *deep sea* yalikuwa hayafiki serikalini ndiyo tatizo kubwa lilokuwa linajitokeza na ndio ilipopelekea kwamba Kanuni zile zitungwe kwa haraka na mapungufu yale yaonekane. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, nimemuelewa sana Mhe. Waziri lakini amekuwa anacheza pia ya kuzunguka. Mimi kwanza sijashughulika kwenye kutunga Kanuni hizi na vile vile najua ninapokwenda, sisemi sijui ninapokwenda kama alivyo *windup issue* yake. Nilikuwa nimekamata fungu hili kwa mnasaba mzima wa kuongeza mapato ya serikali yetu. Sasa ameibua hoja nyengine ya kusema mapato yalikuwa hayafiki serikalini yalikuwa yanakwenda wapi. Mhe. Mwenyekiti, tuendelee. Nataka kumpa indhari tu.

Kifungu A0111	Idara ya Maendeleo ya Uvuvi	3,050,000,000
	Jumla kuu ya A01	**12,500,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU A01 - WIZARA YA KILIMO MALI ASILI MIFUGO NA UVUVI

Kifungu PA0101 Programu kuu ya Maendele ya Kilimo

Mhe. Mohammed Said Mohammed Dimwa: Mhe. Mwenyekiti, wakati nikichangia nilionesha kusikitishwa sana na jitihada kubwa zinazofanywa na Rais wetu Dkt. Ali Mohamed Shein ya kuwa na miundombinu ya umwagilia maji katika sekta zote. Lakini kitu ambacho kinanisikitisha sana 2017/2018 ilipangwa shs.27,056,760,000 lakini safari hii imepangwa shs.9,985,766,000 niliona sana tunakwenda kupunguza. Kwa nini pesa hizi zilipunguzwa na mradi huo hatujaambiwa kama tayari ume-*take off* au uko vipi. Nilikuwa naomba ufafanuzi.

Mhe. Waziri wa Kilimo Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, kama alivyoeleza Mhe. Mohammed Said Mohammed Dimwa ni kweli kwamba kwanza mradi huo nataka nimuhakikishie kuwa suala la umwagiliaji maji tumelipa kipa umbele sana, tunajua kwamba hii ndiyo pekee ambayo itatuokoa katika kilimo cha mpunga na hivi sasa tumo katika taratibu za kuhakikisha kwamba mradi huu utasimamiwa na kufadhiliwa na Kampuni ya Korea unaweza ku -*take off* wakati wowote (*KOICA*).

Kwa hivyo wakati wowote ule mradi unaweza ukafanya kazi na ndio maana tukaweka bajeti hii, kutoka bajeti hii iliyowekwa mwaka jana ambayo iiyokuwa hai ku-*take off,* bajeti ya mwaka ya mwaka huu haina tatizo lolote inaweza ikafanya kazi.

Mhe. Mohammed Said Mohammed Dimwa: Mhe.Mwenyekiti, nimemuelewa sana Mhe Waziri anaposema wakati wowote inawezekana miaka sita, miaka miwili, miaka mitatu lakini *commitment* ya serikali katika bajeti hii anamalizia bajeti ya inayokuja haiwezi kuweka kifungu hapa tena, tunataka *commitment* ya serikali.

Mhe. Waziri wa Kilimo Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kama Mhe. Mjumbe anavyojua kwamba miundombinu tayari imeshawekwa, *commitment* za wizara ni kuhakikisha kwamba kitu hiki kinamalizika na nilipomwambia wakati wowote kwamba kitu hichi kitafanyika kwamba *process* zinaendelea. Kwa hivyo tunamuomba tu aziache wizara iendelee na *process* zake zikimalizika siwezi kumpa tarehe fulani kwamba litakuwa limemalizika, lakini hatua ziko nzuri na tunaendelea kulifanyia kazi.

Mhe. Mohammed Said Mohammed Dimwa: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu sana Mhe. Waziri labda tulibishana kilugha, yeye alizungumza lugha ya Uroa zaidi, akawa sikumfahamu vizuri sana lakini nataka kumwambia ikiwa wakati wowote inaweza kuwa hata mwakani lakini mimi nasema bajeti ijayo iwe haipangwi pesa ya mradi huu ambayo imeshakamilika na akilijibu hilo na tuendelee.

Kifungu PA010

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii leo nikaweza kusimama ambapo mchango wangu niliupeleka kwa Mhe. Waziri kwa njia ya maandishi, najua kutokana na muda na pale penye kiriri, Mhe. Mbunge wa Chwaka, Mhe. Baguanji Mshamba alisema huwa pana setani. Kwa hivyo wakati mwengine huwa anaweza akasahau akapitikiwa.(*Kicheko*)

Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikitoa mchango wangu wa maandishi nilimuomba Mhe. Waziri aweze kutoa kauli ya kufuta Kauli ya Serikali ambayo kauli hiyo ilitolewa na Mhe. Waziri wa Kilimo aliyekuwa Mhe. Hamad Rashid Moh'd ambayo aliahidi kwenye Baraza lako hili Tukufu kwamba baada ya miaka mitatu Zanzibar haitoagizia tena mchele, kwa sababu tumekuwa tumejitosheleza kwa mpango wa kilimo cha umwagiliaji maji.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kila nikija nilikuwa nahesabu miaka. Sasa leo ile siku ambayo aliyoahidi imefika, miaka mitatu imefika bado Zanzibar tunaagizia mchele. Kwa hivyo nimesimama kwa Kanuni ya 37, lakini vile vile nguvu yangu, hoja yangu inatiliwa nguvu na Kanuni ya 59 na kwa sababu kwa pamoja kwamba Mhe. Hamad Rashid Moh'd hayupo lakini serikali inafanyakazi kwa pamoja kama Kanuni yetu ya 37 inavyosema.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba kauli ya Mhe. Waziri kwa sababu yeye ndiye aliyerithi kiti hicho basi aidha kama lile suala alipitikiwa, basi aliombe radhi Baraza ili ile *hansard* ya Mhe. Waziri wa Kilimo ifutwe, kwa sababu Waziri wa Kilimo bado yupo. Ahsante Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Kilimo Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza kabisa nikubaliane kwamba Mhe. Hamza Hassan Juma alileta mchango wake kwa maandishi na kweli nimeusoma huo mchango, lakini nataka nimuhakikishie kwamba maana ya kupanga hii bajeti, serikali hupanga mpango ambao unatarajia kuutekeleza kwa ajili ya kuwahudumikia wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, na pale inapopanga mpango unaweza ukafikiwa kwa asilimia zote, unaweza ukawa unamapungugu kidogo katika kufikia zile asilimia, lakini wakati Mhe. Waziri alipokuwa akiwasilisha bajeti ile miaka mitatu iliyopita, alikuwa anajua ni mpango ambao unaweza kutufikisha kuepukana na suala la kuagizia mchele hapa Zanzibar. Nataka nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi, Hamza Hassan Juma na mimi Rashid Ali Juma, babu yetu mmoja na majimbo yetu yamepakana kidogo katika maeneo mengi ambayo tunashirikiana.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyeiti, nataka nimuhakikishie Mhe. Hamza kwamba Zanzibar ina dhamira hii muda mrefu. Mnamo mwaka 1978 aliyekuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti Baraza la Mapinduzi Mhe. Aboud Jumbe Mwinyi aliliweka eneo la Kilombero hekta 560 kwa ajili ya kilimo cha Mpunga na kwa wakati ule, alipoileta Kampuni ya Kichina kuja kufanyakazi ya kumwagilia pale eneo la Kilombero, Zanzibar ilivuna mpunga na tukajitosheleza, ulibakia mpunga maeneo ya Kizimbani ikawa ni chakula cha panya badala ya chakula cha binadamu.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo uwezekano wa kutumia ardhi yetu tukifuata masharti ya kilimo serikali yetu inaweza ikasimamia na tukaweza tukalima na tukaweza tukafika hatua ya kuweza kujitosheleza chakula na tutakapo kigeuza kilimo kuwa sehemu ya bishara basi tunaweza tukauza hata nje ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo Mhe. Hamza kuifuta Kauli ya Serikali, nia ya serikali haikosei, tulipanga bajeti, mipango ni kupanga na kupangua. Ninataka nikuhakikishie kwa ukaribu wako uliokuwa nao Mhe. Hamza na Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Amani, tutakaa pamoja tusaidiane

maarifa ili tuwaokoe wananchi wa Zanzibar warudi katika kilimo waweze kulima na waweze kujitosheleza na kilimo kiwe na faida ya biashara kwao.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo kauli hiyo Mheshimiwa naomba tuiwache kidogo, tuitizame angalau upite wakati, tupe kidogo muda mrefu hivi tupite tutizame, ndio tofauti sababu ya bajeti na ndio maana bajeti ukapanga kinachobakia unaki-*hold* unakipele *new break forward* mwaka unaokuja.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo bado mipango ipo, nataka nimuhakikishie kuwa mradi huu unaokuja wa Korea ambao tayari tumeshautangazia tenda, tukiweka miundo mbinu tuliyokuwa nayo, robo hekta tuliokuwa tunazalisha gunia mbili za mpunga, sasa tunazalisha gunia nane za mpunga, naamini tunaweza tukafanikiwa na tukafika huko. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo bado wacha niibebe kauli hiyo Mhe. Hamza nakuomba unisaidie niwache niibebe hiyo kauli na wewe kama Mwakilishi mwenzangu tushirikane moja kwa moja tuweze kuhakikisha kwamba tunasaidia Serikali yetu ya Mapinduzi chini ya uongozi mahiri wa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. *(Makofi)*

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri wa Kilimo, Maalimu Rashid mimi ni rafiki yangu sana. Lakini namuomba hii kauli huu mzigo asiubebe. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, kauli aliyoitoa Mhe. Hamad Rashid Moh'd ilikuwa ni kauli nzito sana kwa chombo chetu cha Baraza la Wawakilishi, kama angelisema tunategemea, tunarajia, ingelikuwa ni sawa, lakini alisema baada ya miaka mitatu kama Zanzibar itaendelea kuleta mchele atajiuzulu.

Mhe. Mwenyekiti, sasa ndio maana nikamwambia Mhe. Waziri huu mzigo asiubebe, kwa sababu mimi sipendi ajiuzulu Mhe Waziri. Mimi nadhani Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu lazima tutafautishe, tena ningependelea sana Mhe. Hamad Rashid Moh'd angelikuwepo leo ili kauli angeilitoa yeye mwenyewe, kwa sababu tutofautishe baina ya Baraza na barza. Hili ni Baraza la Wawakilishi linaongozwa na Kanuni na Kanuni ya 59 Mhe. Mwenyekiti, labda niisome ili nisionekane labda nazungumza kwa utashi.

Mhe. Mwenyekiti, Kanuni ya 59 naomba niisome:

" (3) Mjumbe yeyote anapokuwa akisema Barazani atawajibika kuwa na sababu za msingi kwamba maelezo anayoyatoa ni sahihi na sio mambo ambayo ya kubuni au ya kubahatisha tu, na Spika na Mjumbe mwengine yeyote anaweza kumtaka Mjumbe huyo anayoyasema uthibitisho wake kwa uhakika kwa yale anayoyasema".

Mhe. Mwenyekiti, Sasa Mhe. Mwenyekiti, hapa Mawaziri wote wanatoa ahadi lakini hawafiki pahala wakafikia tamati, yeye alijifikishia tamati, kama Zanzibar itaagizia mchele baada ya miaka mitatu kutoka ile siku ambayo aliyozungumza yeye atajiuzulu.(*Makofi*)

Sasa hii kauli nzito. Sasa tunataka ile kauli aidha ifutwe au hapa Mheshimiwa awajibike. Hapa hakutekeleza ahadi yake. Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Waziri wa Kilimo Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe Mwenyekiti, ahsante sana naendelea kumpongeza sana Mhe. Hamza kwa upeo wake ambao anauona, lakini napenda kurejea maneno yangu niliyomwambia kwamba Kauli ya Serikali inabakia kuwa ni Kauli ya Serikali. Dhamira ya serikali ni kuleta bajeti ndani ya Baraza lake tukufu hili, ni kuweka mpango ambao itakwenda kuitekeleza. Kwa hivyo wakati ule alipoji- *commit* Mheshimiwa, aliji-*commit* kwa niaba ya serikali.(*Makofi*)

Mimi nimekwambia kwamba mimi nawewe tusaidiane kuichukua Kauli ya Serikali tuibakishe kuwa ni Kauli ya Serikali ili tuweze kuifanyia kazi.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nataka nikupe takwimu na kukueleza hali halisi ilivyo. Katika mipango ya wizara yangu Mhe. Mwenyekiti, utoaji wa pembejeo kamili ulivyo juu ya mradi wa *ERPP* na mradi wa *EXIM* unaongojea miundo mbinu ya umwagiliaji una uwezo wa kufanya tani 1,524 tuache uvivu, kwa nini tani hizi tusiweze kuzalisha. Kwa nini tuogope kuji-*commit* Mheshimiwa. Mimi ndiyo maana nilichokisema kwamba tukiweza kufanya kazi hii fedha tayari zimeingia zipo na tumeziombea ndani ya bajeti hii.

Mhe. Hamza nataka kukwambia tani 1,524 zikifanyiwa kazi ipasavyo tunaweza tukazalisha tani 193 za mchele, mahitaji yetu ni tani 90,000. Sasa kama mahitaji yetu sisi 90,000 na uwezekano wa kuzalisha tani 193, sisemi kwa nguvu za mtu mmoja tu zinaweza zikapeleka pale lakini nataka liazimie Baraza lako tukufu kamba waniunge mkono, wanisaidie katika kusaidiana kusimamia suala hili ili tulifikishe pale ambapo serikali imedhamiria.(*Makofi*)

Kwa hivyo hiyo Kauli yake, tena nimshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi nasema kwa imani yake aliyonipa mimi mshamba wa Uroa, kuweza kunipa hii wizara na kuweka pale kuisimamia masuala mazima ya kilimo. Mimi nimetoka katika ukulima katika wakulima na wakwezi, mimi nimetoka katika wavuvi. Kwa hivyo naamini Mhe. Hamza atuelewe kwamba ni dhamira ya kutengeneza bajeti, msimamo wa kuweza kujitosheleza kwa chakula iwe samaki, iwe muhogo iwe mchele hivyo vinawezekana naomba tuzitumie vizuri heka 1,524 siji-*commit* na mimi kusema kwamba ndani ya mwaka mmoja kila mtu atakula mchele huu lahasha, lakini serikali ina uwezo wa kuwasaidia wananchi wake ikawapa taaluma, ikawapa elimu ya kutosha ikawasaidia maarifa na ujuzi tukaweza kufikia pahali.(*Makofi*)

Kwa hivyo namuomba Mhe. Hamza tulione tu hili suala la serikali tuisaidie serikali kama tulivyokuja hapa Baraza kuweza kuisaidia serikali ili tuhakikishe serikali inafanikiwa na mchele wa Zanzibar unavyoujua unanukia amesema mchangiaji mmoja hapa, upite barabarani mchele wa Zanzibar zamani unanukia hapa siyo kama mchele tunaouagizia. Nashukuru sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, Waziri hasa hoja yangu hajaijibu na yeye ameeleza mipango atakayoifanya yeye kauli ya Mhe. Hamad Rashid ilikuwa *straight forward,* “kama Zanzibar itaendelea kuagizia mchele nitajiuzulu”.

Sasa ina maana kama hiyo Kauli ya Serikali basi itabidi tusubiri bomba labda jioni, eeh! maana yake bomba jioni saa tisa ikifika tuambiwe kwamba kiti cha Mhe. Hamad Rashid kipo wazi.

Kwa sababu hili ni Baraza na ndiyo maana Baraza hili chochote utakachokisema kinabakia *hansard.* Mimi nimezisoma *hansard* toka za Mhesahimiwa Marehemu Mhe. Fadau ndiyo maana Baraza la Wawakilishi ndiyo sisi tunawalipa watu kwa ajili ya kazi ya *hansard* tu kuweka maneno ambayo tuliyoyasema na ndiyo maana mtu anaambiwa kama umetoa kauli isiyofaa unatakiwa uombe radhi ili ifutwe. Sasa leo Mhe. Hamad Rashid kaji-*commit* hapa Barazani ile ni kauli nzito kwa Baraza. Mimi naomba ile kauli isibebeshwe serikali, ni kauli ya waziri mwenyewe aliyekuwa kabeba ile dhamana.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani sijui labda Mwanasheria Mkuu anaweza kutusaidia katika hili lakini kimsingi kwa kweli ile kauli Mhe. Rashid kwa kweli hakuitendea haki Baraza la Wawakilishi Baraza letu linaendeshwa na Kanuni. Naomba nikae Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nataka niendelee *simple arithmetic* Mhe. Hamza Hassan Juma.

Ninafikiri tuzingatie tu na kauli aliyoitoa Mhe. Waziri Hamad Rashid wakati ule ya miaka mitatu, natumaini nayo inakwisha katika mwaka 2018/19 haujamalizika kwa sababu hata sisi ndani ya Uwakilishi wetu huu tangu tuingie humu na tuanze bajeti hatujafika katika utumishi huo wa bajeti tatu za 2018/2019 itakuwa ndio bajeti hii. Kwa hivyo Mhe. Hamza ndio pale nilipoomba Kauli ya Serikali tuibakishe kama bado ya serikali, tusubiri mpaka ifike igote pale koo! ikishagota ile kauli Mhe. Hamza tunaweza tukairudisha kidogo.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hamza Hassan Juma ninadhani tumemsikia Mhe. Waziri na tukubaliane.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, usinilazimishe kukubaliana na Mhe. Waziri tutaangalia *hansard* Mhe. Hamad Rashid alitoa kauli ile tarehe ngapi lakini kilikuwa ni kikao hiki hiki cha bajeti, nadhani kama itakuwa bado labda itakuwa wiki moja. Kwa hivyo sisi au mimi baada ya wiki moja nitaangalia meli pale bandarini kama kuna meli zinateremsha mchele basi itabidi Mhe. Spika amzuie Mhe. Hamad Rashid asiingie humu Barazani mpaka afute kauli yake. Hii ni *commitment.*

Mhe. Mwenyekiti, naomba tutaendelea lakini hii kauli naomba aje aifute yeye mwenyewe hapa Barazani. Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mjumbe tunaendelea.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nimeinuka huku.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe humo katika orodha yangu. Mhe. Ali Khamis Bakar. Mhe. Jaku kaa kitako kwanza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona na nimshukuru sana Mhe. Waziri alipokuwa akifafanua hoja alitaja hoja yangu na nilipeleka mchango wangu kwa maandishi kuhusu *vote* ya Kitengo cha Matrekta.

Kitengo hiki ni muhimu sana kama kweli tunataka kusaidia kilimo na kama hakupewa kitengo hiki huyu itakuwa mtihani. Nimuombe Waziri hili limeshapita tugange lijalo, sina nia ya kuzuia kifungu. Je, atakayejaaliwa kuwa Waziri huko mbele, nataka Kauli ya Serikali itatengewa *vote* yake maalum. Vyenginevyo matrekta yanaharibika, mabonde inakuwa mtihani tutamlaumu huyu na huyu ni Katibu Mkuu mzuri kupita kiasi ana uzoefu wa mambo ya kilimo.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mjumbe. Mhe. Waziri majibu.

Lakini Waheshimiwa Wajumbe mnapochangia hata kwa maandishi lazima tueleze dhamira yetu wakati wa kupitisha vifungu ili na huku kwenye kumbukumbu ziwepo, ukipeleka kwenye maandishi huku hakuna basi itakuwa haieleweki. Naomba utaratibu tuutumie. Mhe. Waziri endelea.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti nakushukuru kwanza kwa muongozo wako, ni kweli Mhe. Jaku Hashim ameleta mchango wake kwa maandishi bila ya kueleza dhamira yoyote juu ya kifungu hicho. Lakini napenda kumuhakikishia tu kwamba azione jitihada za serikali tumefufua matrekta hadi hivi sasa tuna matrekta 47 ambayo yanaweza kuingia ndani ya bonde lolote kufanya kazi.

Kwa hivyo serikali imeweka mpango mzuri katika bajeti na ombi alilolileta tumesema tunalichukua na kwa mwakani tutalifanyia kazi. Lakini tunakwenda kwa mujibu ilivyoundwa ile Sheria iliyounda Mamlaka ya Matrekta. Hivyo kwa mujibu wa ile sheria na kwa mujibu wa taratibu zilizokuwepo mwaka huu kama alivyosema aliache mwakani tutalizingatia na sisi tutazitizama na sheria zinavyoruhusu ili tuliwekee voti kama vile anavyosea.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nikubaliane nae Mhe. Waziri nia ya serikali ni nzuri sana na tumeona serikali imenunua matrekta mapya kabisa. Kwa hivyo jambo la kushukuru sana chini ya utawala wa Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein. Lakini hata Kamati ya Fedha, Biashara, Kilimo ilikuwa na malalamiko kama mtu hajawezeshwa itakuwa mtihani, hivyo aiweke sawa tu Kiswahili mwakani panapo majaaliwa hiki Kitengo tukisaidie, kasema atalifikiria kufikiria anaweza kukubali au kukataa. Mimi nataka *commitment* kuwa panapo majaaliwa kama si yeye Waziri atakayekuja iwe *hansard* ikae sawa tu kwa hili suala ni muhimu na lina uzito wa aina yake. Vyenginevyo tutakuwa tunatwanga maji kwenye kinu.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Jaku umeshasikika.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, nataka kukujulisha kwamba Mhe. Jaku Hashim naye aendelee kukisoma hiki kitabu sitaki kusema maneno mengi. Hiki kitabu akisome tumepewa hiki kitabu ili tutizame voti baada ya voti, nimekwambia kwa

bajeti hii ya serikali sisi tumelizingatia hilo na tumeweka hapa voti “huduma za matrekta zenye na zana nyenginezo voti SL010105 ina jumla ya bilioni 1 milioni 568”, sijui kama wataweza kuzitumia zote hizi wakati matrekta yapo mengi mazima.

Kwa hivyo Mheshimiwa namwambia tu kwamba ule ushauri wake anachokitaka kama kuongeza kwa mwakani tutaongeza tutatizama na hali na sisi lengo letu lote sisi tuweze kuweka mageuzi katika kilimo.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea Mhe. Jaku.

Kifungu PL 0101 Programu kuu ya Maendeleo ya Kilimo 19,111,043,000
Kifungu PL0102

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Suleiman Sarahan Said sioni jina lako katika watu ambao wamesema watazuia fungu.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, nilichangia mashamba ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti: Nia haikusikilikana kwamba utazuia fungu.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Niliweka nia nikasema kwamba Waziri atakapokuja anieleze. Nilisema hayo, nataka ufafanuzi tu sina nia ya kuzuia fungu, nilisema nataka ufafanuzi wa mashamba yaliyokodishwa na Serikali, nilisema. Sikusema nazuia fungu, nilisema nataka ufafanuzi na Waziri hakutoa.

Mhe. Mwenyekiti: Endclea tu.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, wakati nachangia nilisema kwamba kuna maneno mengi sana kule Pemba kuhusu habari ya mashamba ya karafuu yaliyokodishwa kuna watu hawajalipwa kuna watu wana matatizo tele. Nikamuomba Mhe. Waziri kwamba akija anieleze tumefikia wapi kuhusu haya matatizo, maana yake wengine ni waongo wengine wanaipaka matope serikali. Sasa nilimuomba Waziri kweli kuna watu hawajalipwa au kuna kitu gani katika mashamba ya mikarafuu.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi nataka nikiri ni kweli Mheshimiwa kaeleza suala hilo na suala hilo kweli ni nyeti linagusa wananchi linagusa wanyonge linagusa watu ambao wanazalisha kwa kiasi kikubwa pato la nchi yetu, Kwa hivyo nakubaliana na suala lake na umuhimu wa suala hilo, lakini nataka nimjulishe tu kwamba mpango tayari umekuwa upo katika hali nzuri. Mheshimiwa majina tumeyapeleka tayari na kwa kiasi mpaka idadi ya fedha ambazo zitalipwa chini ya Wizara ya Fedha tayari zimesainiwa. Kwa hivyo wale wote ambao wanatakiwa kulipwa watalipwa namuhakikishia tu chini ya usimamizi wetu haki itatendeka.

Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Ahsante Mheshimiwa nimeridhika na kauli yake.

Kifungu PL0102	Program kuu ya Maendeleo ya Rasilimali za Misitu na Maliasili Zisizorejesheka	2,431,567,000
Kifungu PL0103	Programu Kuu ya Maendeleo ya Mifugo	

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Maryam Thani Juma hapa sijaona jina lako kama na wewe ulisema utazuia fungu. Kwa hivyo wache tuendelee.

Mhe. Maryam Thani Juma: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia kwa maandishi nilisema namtaka Waziri anipe ufafanuzi.

Mhe. Mwenyekiti: Katika orodha yangu hapa sina, sijapata taaarifa hiyo.

Mhe. Maryam Thani Juma: Ndio ninataka ufafanuzi nimeandika hayo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri mjibu.

Mhe. Maryam Thani Juma: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nimesema kwamba shamba lililopo Mziwengi Gando mwaka 2014 wananchi hao walitathminiwa fidia za vipando vyao na kwamba watalipwa na kwenye kitabu hiki tumeambiwa kwamba wataweka uzio katika shamba lile, lakini ukizingatia tathmini tayari imeshafanyika na hapa tumeambiwa utajengwa uzio na nyumba tayari imeshajengwa katika eneo hili. Je, Mhe. Waziri naomba uniambie lini watalipwa fidia za vipando vyao.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza sijamfahamu kama ninachokisema katika fungu tulilokuwepo.

Mheshimiwa tumepewa bajeti na bajeti tatizo pengine inaandikwa kwa namba tu maneno yanakuwa machache hesabu inakuwa ndiyo nyingi. Kwa hivyo hapa tulipo tupo PL0103. Sasa sijui kama hicho kifungu chake kinaelezea suala hili, maana nisijekujibu kupitisha fungu suala jengine na huku tuna suala jengine, naona kama haviendani hivi vitu viwili. Kwa hivyo nisitwange maji kwenye kinu, nijibu lile suala ambalo linakuwa lipo, lakini nakiri kwamba kweli ameleta mchango na hiyo voti imepita huko nyuma imekupita Mhe. Maryam Thani Juma.

Mhe. Maryam Thani Juma: Mheshimiwa tuendelee kama kifungu kimeshapita.

Kifungu PL 0103	Program kuu ya maendeleo ya mifugo	3,665,650,000
Kifungu PL0104		

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kuanza kusema hiki kifungu nilikuwa naomba sana unione ili niweze kutoa ufafanuzi wa bajeti. Wajumbe wakati mwengine wanaomba ufafanuzi siyo kuzuia kifungu.

Sasa wakiomba ufafanuzi wakati Mheshimiwa alikuwa na mambo mengi pale hakuwahi kuyasema, inabidi awape ufafanuzi ili na Kamati yangu ipate kuandika kile ambacho wanakitaka hilo. (*Makofi*)

Lakini sasa nakwenda kwenye kifungu. Mhe. Mwenyekiti, hapa nilikuwa na hoja mbili. Hoja ya kwanza ni kuimarisha uvuvi wa bahari kuu. Mwaka jana walitengewa Shs.3,884,000,400 lakini mwaka huu wametengewa 10,416,000,000. Sasa nilikuwa ninataka kujua hizi pesa za nini hapa mbona zimekuwa zimeongezeka mara mbili zaidi. Hiyo ni hoja ya kwanza.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mheshimiwa naomba arejee kidogo.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mheshimiwa kuna kifungu kidogo HL01040204 "kuimarisha uvuvi wa bahari kuu", mwaka 2017/18 ilipangiwa shs.3,884,000,400 lakini mwaka huu imepangiwa 10,416,000,000. Sasa nilikuwa nataka kujua kimeongezeka zaidi cha nini hiki, pesa hizi za nini.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoeleza kwenye maelezo yangu pale wakati najumuisha. Kwanza serikali yetu sasa ina dhamira ya dhati kabisa kuhakikisha kwamba inaendeleza na inaleta mageuzi katika uvuvi wa bahari kuu. Kwa hivyo ni kweli kifungu hiki kimepanda kwa ajili ya shughuli za utawala za kuhakikisha masuala hayo yanaweza yakafanya kazi vizuri, lakini vile vile masuala ya kufanya doria. Uvuvi wa bahari kuu umekuwa unaonekana kuna mambo mengi ambayo yanakwenda kinyume na masuala yetu ya uvuvi. Kwa hivyo ni wazi kwamba lazima tuweze kui-*support* hili fungu ili tuhakikishe kwamba ulinzi, usalama na kuweza kuitembelea maeneo hayo ya uvuvi yanafanyika.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu sana Mhe. Waziri lakini hapa panakuwa na pesa zake hii Mamlaka wenyewe *per say*, inakuwa na asilimia 50 ilivyosema *operation cost* ambazo inajiendesha wenyewe na yeye mwenyewe katika majibu yake ya mwanzo kabisa alisema kwa upande huu sasa hivi kwa sababu wafanyakazi wote wanalipwa katika wizara zao, lakini pesa inayopatikana hapa ndiyo pesa ya uendeshaji. Sasa hii pesa ya serikali ya nini hapa wakati pesa wanayopata wanayo-*collect* kule inakuwepo.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, natumaini wazi kuwa Mhe. Mjumbe anajua kwamba dhamira ya serikali sasa hivi juu ya kuendeleza suala la uvuvi na ndiyo maana serikali imeweza kuunda Kampuni ya *ZAFICO* ambayo ipo chini ya Wizara yangu ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi katika kuhakikisha kwamba inaendeleza masuala mazima ya bahari kuu. Anaelewa wazi kwamba *ZAFICO* hivi sasa imechangiwa na mashirika lakini bado wizara ina majukumu ya kuweza kuhakikisha kwamba nayo inafanya kazi kwenye bahari kuu kama ilivyopangwa. Kwa hivyo kifungu hiki pamoja anayoyaona lakini katika mageuzi mazima ya suala la kuweza kuiwezesha uvuvi wa bahari kuu kufanya kazi zake pamoja na kununua vifaa, meli kutengeneza mambo mengine bado inaonekana bajeti hii nayo iweze kui-*support* uvuvi wa bahari kuu.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu sana Mhe. Waziri lakini alikuwa hajaainisha kama ile Kampuni ya *ZAFICO* inaingia hapa tukisema tu uvuvi wa bahari kuu hatukuelewi. Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu PL 0104 Program kuu ya Maendeleo ya Uvuvi 20,759,216,000
Kifungu PL0105

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hidaya Ali Makame, Mhe. Miraji Khamis Mussa na Mhe. Hamza Hassan Juma hawa ndiyo waliokuwemo katika orodha ya watu ambao walisema wanataka maelezo kwenye kifungu hichi. Mhe. Hidaya Ali Makame endelea.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia kwa maneno lakini na hata mchango wangu wa maandishi nilionesha nia ya kuzuia fungu hapa. Kwanza wakati nikichangia kwa maandishi nilimuomba Mhe. Waziri na nikamtaka aje atwambie kuhusiana na suala la shughuli za Siku ya Chakula Duniani, nikamwambia kwamba nikamuomba sana kwamba suala hili aje atwambie kutakuwa kuna utaratibu gani juu ya suala la kuimarisha maonesho ya vyakula vya asili, lakini pia na banda linalohusiana na masuala ya maonesho ya mifugo na uvuvi pia. Hivyo hakunipa majibu yoyote wala ufafanuzi wowote. Ningemuomba sana Mhe. Waziri hapa anifafanulie hilo suala langu lakini pia naendelea kuzuia fungu hili hili kwa mchango wangu wa maandishi Mhe. Mwenyekiti, sijui nieleze kabisa.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo, Maliasili na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, niendelee kukiri na kukubali kwamba kweli Mhe. Hidaya wakati akichangia mubashara alieleza suala hili na ninamshukuru kuniambia wazi tu maana na bajeti ya jana ilikuwa ni muhogo na samaki ijapokuwa tumefunga.

Lakini Mhe. Hidaya napenda kumjulisha kwamba suala la maonesho kama tulivolianzisha ni suala endelevu, nimetumia fursa jana kuweza kuhakikisha kwamba nawaalika Waheshimiwa Wawakilishi wote katika maonesho ya mwaka huu ambayo yatakuwa ya aina yake maonesho ya kilimo. Mhe. Mwenyekiti, tunapofanya maonesho yale vyakula vya asili vinakuwepo. Mara ya mwisho sisi tumekula vyakula ambavyo tumevisahau mpaka miaka kumi na tano ishirini iliyopita, makopa, vipopoo vya muhogo vingi sana tumekula, lakini vile vile katika maonesho ya mazao ya baharini yanakuwepo. Ni mwaka jana maonesho yaliyopita Mhe. Mwenyekiti, nimeweza kushuhudia samaki mkubwa aliyevuliwa aina ya jodari mwenye uzito wa kilo sabini alikuwepo pale kwenye maonesho, chaza na makome yalikuwepo ambazo zinapatikana kule sehemu za Nungwi na sehemu nyenginezo.(*Makofi*)

Lakini vile vile kulikuwa kuna usarifu hata wa yale mazao mengine ya baharini, chwale za nazi zilikuwepo katika vyakula vya asili na vitu vyengine kama hivyo. Maonyesho ya safari hii kwa vile inaonekana yamevutia vizuri sana mwaka jana, namuomba Mhe. Hidaya atapata ule mualiko

wa kwanza na yeye atakuwa ndio mtu wa ku-*test* kwa sababu wakati huo itakuwa sio mwezi wa Ramadhani, asiwe na wasi samaki na mazao mengine ya baharini yataendelea kuwepo katika maonesho kama ilivyokuwa maonesho yanafanyika katika mwani. Mambo ambayo yanaingia katika biashara kugeuza mambo mengi mengi ya *branding* kwenye biashara. Ahsante sana.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nampongeza sana na namshukuru sana Mhe. Waziri, lakini tu kwa ile hamu kwa sababu Uzanzibari ndio Mzanzibari halisi na vile vyakula na maonesho na kila kitu, tukiona, tukifahamu na tukizidi kujifunza ndio akili zinazidi kukua. Kwa hivyo hongera lakini aendelee tuje tuyaone vizuri huu mwaka huu kama ulivyotuahidi.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nasimamia hoja yangu nyengine hapa hapa wakati nilipokuwa nikichangia kwa maandishi…

UTARATIBU

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kawaida katika fungu moja kunakuwa na hoja tatu na wewe umeshawatangaza watu watatu. Sasa ina maana Mhe. Hidaya ukimpa hoja ya pili, ina maana wale wengine itakuwa umeshawakosesha. mimi nadhani kwa kuwa umeshawataja ingekuwa hujawataja ungemuacha akaendelea hata akamaliza hoja zote tatu, lakini ndio umeshamtaja na mtu ukishamtaja ukimkosesha inakuwa si haki.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa wote watapata nafasi.

MUONGOZO

Mhe. Nadir Abdul-latif: Muongozo wako Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa naomba ukae, Mhe. Hidaya endelea.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunilinda. Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia kwa maandishi nilionesha nia ya kuzuia fungu kumtaka Mhe. Waziri, ndani ya bajeti hii ambayo tunaendelea kuipitisha leo hii anipe neno au atwambie ndani ya bajeti hii ni fungu gani lililoandaliwa juu ya utekelezaji wa kukarabati zile nyumba za utafiti wa kilimo pale Kizimbani, ikiwemo ya Kijichi, pale Mndo lakini hata pale gereji na zilizokuwepo Chuoni juu kilimo, anambie ni fungu gani lililotengwa na kiasi gani zimewekwa kwa ukarabati wa nyumba ile. Kwa sababu hata mwaka jana niliwahi kulichangia hili na bado sikupata majibu yoyote na mpaka leo nyumba zile iko zinaonekana katika hali ile ile ya uchakavu na uduni. Naomba Mhe. Waziri anipe majibu ahsante.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo, Maliasili na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. jibu lake nilitaje kwa upesi tu ni fungu SL010501. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Mhe. Mwenyekiti, mimi hili fungu nimeshaliona lakini tu kwa niaba ya wananchi wote naomba alisome na atuainishie kwamba fedha fulani ndio zilizotengwa na wananchi ili wasikie na wajue kwamba kweli katika mwaka huu wa bajeti vituo hivi au nyumba hizi zitafanyiwa ukarabati na kweli tutaona na uhakika tutaupata ndani ya mwaka huu Ahsante.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo, Maliasili na Uvuvi:: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, fungu hilo nililomtajia Fungu SL 010501 lina jumla ya shilingi bilioni 2,522,692 lakini hapa katika usimamizi raslimali watu na huduma kwa ujumla, nalo utalikuta lipo fungu hilo hapo milioni mbili ambalo liko katika fungu kuu la utawala na uendeshaji wa kazi za kilimo, maliasili, mifugo na uvuvi. Kwa hivyo katika kazi hizo, matengenezo ya hizo nyumba na vitu vidogo vidogo ambavyo vitaingia katika mkumbo huu.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, tuendelee. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa nawaombeni tusubiri hawa watu ambao nimeshawataka ili kupata nafasi tuweze kuona kwamba na wao wanasemaje pengine hoja yako itaweza kujibika. Mhe. Miaraji Khamis Mussa.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante sana Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mhe. Waziri ametujibu kwa ufasaha na kuna majibu ametwambia tusibiri atayatekeleza nimshukuru sana na mimi kuna maeneo nimenyamaza makusudi kwa sababu najua ameshanifahamu. Lakini katika eneo la uendeshaji na uratibu wa Wizara ya Kilimo mimi nalizungumzia la sera kanijibu vizuri, lakini kuna kukamilika kwa utafiti wa kujua uwezo wa uzalishaji kwa mazao ya embe, machungwa na nazi. Ilikuwa lengo kuu hapa katika bajeti iliyopita ni kuimarisha eneo hili lakini kuja kuchangia pato taifa. Sasa nilitakakuju Mhe. Waziri hakunijibu yale mafanikio baada ya utekelezaji ile azma ya kuongeza hili pato ilipatikana na labda kwa tathmini iliyofanywa ni kwa asilimia ngapi, lakini kama haijapatikana basi pia aniambie changamoto ni nini.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo, Maliasili na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, naona suala lake sikulifahamu vizuri nafikiri angerejea kidogo kwa ufupi tu hivi.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Kwa ufupi tu kuna utafiti ya mafanikio ya utafiti yalipatikana kwenye bajeti ya mwaka 2016/2017 mafanikio ya utafiti lakini kwa mazao nikayataja, embe, machungwa na nazi.

Sasa utekelezaji wake ndio niliokuwa nataka lakini kwa sababu azma ya Wizara yake ilikuwa ni kuongeza pato katika pato lile la kitaifa. Sasa yale mafanikio kwa ujumla tu yamepatikana baada ya ule utafiti katika ule utekelezaji wake, lakini kama haijapatikana changamoto baada ya utafiti au utekelezaji ni nini.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo, Maliasili na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, ninakubaliana na yeye kwamba tunafanya tafiti makusudi ya kutizama matokeo na kupata faida gani juu ya mnachotaka kukifanya. Kwa hivyo matokeo ya utafiti yanayofanywa na Wizara ya Kilimo,

Maliasili, Mifugo na Uvuvi mengi yanaonekana yana mafanikio na yana tija yake. Miongoni mwa mafanikio yanatupelekea kuona kwamba mazao yale yanazaliwa vizuri sehemu gani, mazao yale yanakuwa na uharibifu pengine wa wadudu sehemu gani kujikinga na kitu gani. Ni miongoni mwa mafanikio ambayo yanapatikana katika utafiti, lakini katika tafiti zilizofanyika na mafanikio ambayo yameonekana basi hizo zote tunazichukua kwa pamoja na tunayapeleka kwa wakulima wanaohusika, hususan katika vilimo vile alivyovitaja ili tuone namna gani uzalishaji unakuwa mkubwa na Serikali inapata mapato kutokana na mazao yale.

Kama anavyoona jitihada za Wizara ya Kilimo, misimu hii ya miaka miwili amekuwa akiyaona pengine matunda ya matikiti yametokana na mafanikio ya tafiti zilizofanywa, hakuna miezi inayopishana kila unapopita barabarani matikiti yapo, embe hakuna miezi inayopishana sio kama misimu ilivyokuwa inakuja zamani. Kwa hivyo tafiti hizi zinatokana na utafiti wa kujua kwamba muda wa kupanda vitu hivi, muda gani utakuwa na mazao mengi zaidi kutokana na misimu yetu ilivyo. Kwa hivyo tafiti hizo zinapatikana na zinaendelea kufanywa kwa wingi zaidi ndani ya Wizara yetu.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, yawezekana Waziri kanifahamu mbali zaidi. Mimi nilisema tafiti zikishafanyika lakini azma ya Serikali au Wizara yako ni kuongeza kuchangia pato la taifa letu la Zanzibar, mimi ilikuwa anijibu tu ile azma imefanikiwa la kuchangia hili pato na kama haijafanikiwa changamoto ni nini basi.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Mifugo,Maliasili na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mweyekiti, na kweli ndio maana pale nilipomwambia arejee ili niweze kumfahamu vizuri zaidi. Lakini nataka nimthibitishie kwamba faida imepatikana tena kubwa ndio maana katika bajeti yetu hii kunaonekana wazi kama atafungua ukurasa wa L0122 wakati tulipokuwa tukielezea mapato ambayo tutayakusanya mwaka huu, note ya L0109 ambayo ni Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Kizimbani inaonekana mwaka jana kwa kazi nzuri za utafiti mapato yalikuwa ni shs.70,000,000 lakini mwaka huu kwa jinsi inavyoonekana hali nzuri iko milioni 140, *double* ya hii. Kwa hivyo mafanikio yapo vizuri sana kwa Serikali na pato la mchango wa taifa.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti nimshukuru sana Mhe. Waziri tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hamza Hassan Juma kwa kifupi.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nampongea sana Mhe. Waziri kweli inaonesha yeye ni kiungo mkabaji maana yake anavyojibu masuala utafikiri labda hii Wizara yupo tokea mwaka 2002.

Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilielezea kadhia iliyokuwepo ya Wizara kuwa na ukwasi au kuwa na ukakasi wa kulipa madeni hasa ya wataalamu wetu baada ya kufanya kazi za tafiti. Suala alililoliuliza Mhe. Miraji Khamis Mussa sasa hivi linaowana sana baada ya huu utafiti wao matokeo ya utafiti ndio wanayafanyia kazi. Lakini kwa bahati mbaya wale ambao waliofanya hizo tafiti mpaka leo kuna madeni wanadai, kuna kampuni inaitwa *MK. Business Consultancy* ambao wao walifanya *Consultancy Service for the Preparation environmental and Social Impact Assessment for Zanzibar Irrigation in Infrastructure Project*.

Sasa hii Mhe. Mwenyekiti, kuna deni ambalo lililobakia kama nilivyosema Mhe. Waziri ni mahiri sana tena anaweza ku-*clear* mambo yote tena katika hali *very smooth.* Kwa hivyo naomba basi anipe jawabu ili sasa tujue kwamba hawaliofanya huu utafiti hili deni lao watamaliziwa lini, kwa sababu zimeshapita bajeti kama sita bado wanaendelea kuhangaika wanadai lakini kazi yao sasa hivi ndio Wizara wanaifanyia kazi kwa mipango yao ya maendeleo ahsante.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa namuomba Mwanasheria Mkuu ili aweze kutengua Kanuni ya muda tuweze kumaliza Wizara hii kwa muda mdogo ambao umebakia.

KUONGEZA MUDA WA BARAZA

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti nakushukuru, kwa kuwa bado shughuli za Baraza hazijamalizika na muda ambao umetengwa kwenye Kanuni ya 23 ua kumaliza Baraza wakati wa kipindi cha Ramadhani saa sita. Hivyo, naomba nitoe hoja ya kutenga kando hiyo Kanuni ya muda ya 23 ili tutoe fursa kwa Wajumbe kuendelea kwenye Kamati ya kupitisha mafungu mpaka hapo tutakapomaliza hoja hiyo. Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Hoja imetolewa naomba kuwauliza wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Mwanasheria Mkuu wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

KAMATI YA MATUMIZI

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii kukupongeza sana kwa umahiri ambao umekuwa unaendelea kuuonesha kila siku katika kiti chako.

Mhe. Mwenyekiti, pia nimshukuru Mhe. Hamza Hassan kwa neno moja tu, hodari wa kutafuta na hodari wa kupata. Namshukuru sana Mhe. Hamza kwa kazi kubwa aliyoifanya, sio kwamba anatetea makampuni tu lakini hodari wa kutafuta na kuzijua taarifa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Wizara ya Kilimo sisemi wapi kapitia lakini ni kweli ina madeni mengi na sisi tumeyaona katika kipindi hiki tulichokuwepo. Nataka nimthibitishie kwamba na deni hilo alilolizungumza jana pia tumelizungumza na tumeliona na tumelitaja katika madeni ambayo tutayafanyia kazi. Kwa hivyo Mheshimiwa kama ilikuwa kidogo funguo funguo zimepita ndani ya huu Mwezi wa Ramadhani mimi nafikiri asiwe na wasi wasi tumeliona na

aendelee kunifuata tu tutalifanyia kazi kwa vizuri na madeni mengine tumeweza kuya-*clear*. Nashukuru sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nilisema awali Mhe. Waziri kweli ni kiungo mkabaji, maana yake mimi hoja nimekuja nayo yeye jana tayari keshaikalia sio kuikalia chini ya kiti aah! wameshaifanyia kazi. Kwa hivyo mimi naamini Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri ataweza kulikamilisha hilo ili kuhakikisha na wataalamu wetu hawa wanapofanya kazi za kitaalamu waone serikali yao inawajali ili mara nyengine tuweze kuwatumia.

Mhe. Mwenyekiti, naomba tuendelee.

Kifungu PL0105 -	Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Kilimo	Shilingi 16,650,624,000
	Jumla Kuu:	**Shilingi 62,618,100,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi bila ya mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako liyakubali makadirio hayo kama tulivyowasilisha. Mheshimiwa naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri sasa niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na hoja wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Kuhusu Muongozo. (*Kicheko*)

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa naomba ukae. Waheshimiwa Wajumbe kwanza naomba niwatangazie Wawakilishi wote wa CCM baada ya kumaliza kikao hiki wabakie humu ndani. Tangazo hili linatoka kwa Mnadhimu.

Baada ya hapo niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa uvumilivu wenu na kuweza kuipitisha bajeti hii bila ya mabadiliko sasa niombe kuchukua fursa hii kuakhirisha kika hiki mpaka siku ya Jumatatu, tarehe 04/06/2018 tukijaaliwa.

(Saa 6:00 mchana Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 04/06/2018 saa 3:00 asubuhi)